SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2026/2027

ILIYOWASILISHWA NA
MHE. SULEIMAN MASOUD MAKAME (MBM)
WAZIRI WA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO
ZANZIBAR

MEI, 2026

## YALIYOMO


A. UTANGULIZI ....................................................................................................................1
B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZOCHINI YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO...........................................................................................................................4

C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA. ....................................................................5
Mapato yaliyokusanywa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ..................................5
Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji ..........................................................................................5
Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa Kipindi cha Julai 2025 – Machi 2026. ..............................................................................................................7
Programu za Wizara ..........................................................................................................................7
Programu ya Maendeleo ya Kilimo ......................................................................................................8
Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji.....................................................................................8
Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula. .....................................................................9
Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu ..................................................................................10
Programu ya Maendeleo ya Mifugo ....................................................................................................11
Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo .........................................................................................................11
Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo ....................................................................12
Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ..........................................12
Mipango na Uratibu wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo.............................................................13
Uratibu na Uendeshaji wa Ofisi Kuu Pemba .........................................................................................13
Fedha Zilizopatikana kwa Kipindi cha Utekelezaji ...............................................................................14
Utekelezaji wa Vipaumbele kwa Mujibu wa Mpango Mkakati wa Wizara na Taasisi...............................14

D. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2025 - MACHI 2026. ...................................................................................................................................15
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar – ZALIRI ......................................................................15
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ..............................................................16

E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ....................................................16
Mwelekeo wa Mapato ........................................................................................................................16
Mwelekeo wa Matumizi 2026/2027.......................................................................................................16
Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. ..........................................................................17
Mwelekeo wa Programu za Wizara .......................................................................................................18
Programu ya Utawala na Uratibu wa Wizara ya Kilimo...........................................................................18
Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ...........................................18
Mipango na Uratibu wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo..............................................................19
Uratibu na Uendeshaji wa Ofisi Kuu – Pemba .........................................................................................19
Programu ya Maendeleo ya Kilimo .........................................................................................................19
Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji.......................................................................................19
Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula ............................................................................20
Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula. ...........................................................................................20
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar (ZALIRI). ......................................................................20
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo................................................................20

Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu ........ 21
Programu ya Maendeleo ya Mifugo ........ 22
Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo ........ 22

F. MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 . ........ 22
Muhtasari wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. ........ 23
Shukurani ........ 23

G. VIAMBATANISHO ........ 26
Kiambatanisho Nam. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2024 -2025, Zanzibar ........ 26
Kiambatanisho Nam. 2A: Uzalishaji wa Mayai na Maziwa, 2025. ........ 27
Kiambatanisho Nam. 2B: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchinjwa, 2025 ........ 28
Kiambatanisho Nam. 2C: Idadi ya Kuku waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2025 ........ 29
Kiambatanisho Nam. 2D: Idadi ya Wanyama Wengine waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2025. ........ 30
Kiambatanisho Nam. 3: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2025. ........ 31
Kiambatanisho Nam. 4: Ukusanyaji wa Mapato, Julai 2025 - Machi 2026 ........ 32
Kiambatanisho Nam. 5: Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2025 Hadi Machi, 2026. ........ 33
Kiambatanisho Nam. 6A: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027 ........ 35
Kiambatanisho Nam. 6B: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027. ........ 36
Kiambatanisho Nam. 7A: Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji ........ 38
Kiambatanisho Nam. 7B: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania – Kilimo P4R ........ 40
Kiambatanisho Nam. 7C: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula ........ 42
Kiambatanisho Nam 7D: Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi (Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba) ........ 43
Kiambatanisho Nam 7E: Mradi wa Kuimarisha Miundombinu na Uwezo wa Utafiti wa Kilimo Maliasili na Mifugo ........ 45
Kiambatanisho Nam. 7F: Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR ........ 46
Kiambatanisho Nam 7G: Mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Mimea (Botanic garden) na mashamba ya Serikali ........ 47
Kiambatanisho Nam 7H: Mradi wa Ulinzi wa Misitu ya Mwambao wa Zanzibar kwa Manufaa Mchanganyiko ........ 48
Kiambatanisho Nam. 7I: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu ........ 49
Kiambatanisho Nam. 7J: Mradi wa Mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi ........ 50
Kiambatanisho Nam. 8: Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Programu kwa Mwaka 2026/2027 ........ 51

**HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha kwa Baraza Lako Tukufu mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027, ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa Programu (PBB). Aidha, bajeti hii ni mfano wa bajeti inayozingatia jinsia (GRB) na inakusudia kutekeleza Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (2025 - 2035) unaolenga upatikanaji wa fursa za kilimo-biashara kwa vijana, wanawake pamoja na watu wenye mahitaji maalumu.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia leo tukiwa wazima na wenye afya njema ili tuweze kujadili makadirio ya bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar, ambapo inakadiriwa kuwa asilimia kubwa miongoni mwao hujishuhulisha na kazi za kilimo, ufugaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili na mazingira.

3. **Mheshimiwa Spika,** pili napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa tena na wananchi wa Zanzibar kuiongoza awamu ya nane (8) – kipindi cha pili, huku wakijivunia uweledi, hekima na busara zake. Vilevile, nampongeza Mhe. Rais kwa kuendelea kutoa miongozo ya kusimamia vyema utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Utekelezaji huu umeweza kufikia malengo yaliyowekwa kwa zaidi ya asilimia mia moja na mafanikio yaliyopatikana yameisaidia kwa kiasi kikubwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuleta maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Umawagiliaji, Maliasili na Mifugo sambamba na kuongeza tija kwa wananchi na kukuza uchumi. **HONGERA SANA Mh. Rais.**

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuingoza na kuisimamia Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo. Naahidi kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na uzalendo pamoja na kuitumikia Serikali hii kwa uwezo wangu wote, kwa kutekeleza kwa vitendo ILANI ya Uchaguzi ya CCM ili kuleta mageuzi chanya katika sekta ya Kilimo nchini.

5. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuendelea kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na kumshauri vizuri Mhe. Rais katika kuendeleza sekta ya kilimo. Kwa dhati na heshima kuu ninamshukuru kwa maelekezo na miongozo anayoitoa kwa sekta hii yenye azma njema kwa nchi na wananchi.

6. **Mheshimiwa Spika,** halikadhalika nakupongeza wewe binafsi kwa umakini na umahiri wako wa kuliendesha Baraza la Wawakilishi, pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaokusaidia kuliongoza Baraza hili na tunawaombea dua Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo, hekima na busara ili mpate wepesi wa kuliendesha Baraza kwa ufanisi na mafanikio zaidi.

7. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Utalii, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake shupavu Mheshimiwa Fatma Ramadhan Mandoba, Mwakilishi wa Viti Maalum UWT Mkoa wa Magharibi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushauri na miongozo wanayoitoa kwa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo katika kufanikisha utekelezaji wa malengo kwenye bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/2026. Aidha, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Pangawe, pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2026/2027. Napenda kukuhakikishia kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo waliyotupatia tumeyazingatia na kuyaweka katika bajeti hii ninayoiwasilisha.

8. **Mheshimiwa Spika,** mwisho, lakini sio kwa umuhimu, natumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Chonga kwa kunipa mashirikiano na kuwa pamoja nami katika suala zima la kufanikisha maendeleo ya Jimbo letu na nchi kwa ujumla. Naahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta tija na maendeleo Jimboni mwetu.

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo inaendeleza Mipango na Mikakati iliyoanzishwa na Serikali katika kuendeleza Sekta ya Kilimo ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapunguza utegemezi wa mahitaji ya chakula; kwa kuendeleza kilimo-biashara katika uzalishaji na usarifu wa mazao ili kuwawezesha vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalumu kuzifikia fursa za kilimo katika minyororo ya thamani. Juhudi nyengine ni kuimarisha uzalishaji wa mazao ya viungo, mboga na matunda pamoja na mazao ya mizizi ambayo ndio chachu ya maendeleo katika sekta za utalii na viwanda na kuendeleza uzalishaji wa zao la nazi na karafuu. Vilevile, upatikanaji mzuri wa huduma za mifugo ikiwemo udhibiti wa maradhi, utoaji wa elimu kwa ufugaji pamoja na uzalishaji bora wa mifugo utaendelezwa. Pia, Wizara hii itaendelea na usimamizi wa rasilimali za misitu ya hifadhi za Serikali na Misitu ya jamii kwa lengo la kuhakikisha uhifadhi wa bioanuai, mazingira, matumizi endelevu pamoja na kuimarisha uwekezaji katika miradi endelevu ya utalii wa kimaumbile.

10. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inayojumuisha mazao, mifugo pamoja na maliasili za misitu, wanyamapori na nyuki bado ni tegemeo kwa uchumi wa Zanzibar, inayotoa mchango mkubwa katika ajira (asilimia 35 ya wananchi) na inakadiriwa kutoa utegemezi

wa kujikimu kimaisha kwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi. Lengo kuu la Wizara ni kuhamasisha wakulima kubadilisha kilimo chao kutoka cha kujikimu kuwa cha kibiashara kupitia kuongeza uzalishaji kwa teknolojia za kisasa, usarifu, masoko ya uhakika, uhifadhi wa maliasili na mazingira unaolenga kukuza uchumi wa jamii na pato la Taifa. Kwa mwaka 2025 Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia ya 23.5 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 24.3 ya mwaka 2024, 24.9 ya mwaka 2023, 25.9 ya mwaka 2022 na 27.1 ya mwaka 2021. Hii inaonesha kuendelea kuimarika kwa sekta ya Kilimo kwa miaka mitano (5) mfululizo ambapo imekuwa ikichangia katika Sekta nyengine zinazohudumiwa kupitia kilimo kwa malighafi; na ni alama nzuri kwa ukuaji wa uchumi wetu usioongozwa na sekta ya kilimo.

11. **Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kwamba jumla ya eneo lililopandwa mazao ya kilimo limeongezeka kutoka ekari 104,667.8 za mwaka 2024 hadi kufikia ekari 124,357.93 mwaka 2025, sawa na ongezeko la ekari 19,690.13. Kati ya eneo hilo, ekari 99,005.56 ambazo ni sawa na asilimia 79.61 zilipandwa mazao ya chakula. Zao la mpunga lilipandwa ekari 30,145.90 ambazo ni sawa na asilimia 24.24 ya eneo lote lilopandwa mazao kwa mwaka 2025, zao la muhogo lilipandwa ekari 30,515.43 ambazo ni sawa na asilimia 24.54, na zao la ndizi lilipandwa ekari 8,628.48 ambazo ni sawa na asilimia 6.94 **(Kiambatanisho Nam. 1)**. Hivyo, Wizara inaendelea na juhudi za kuhamasisha wakulima kulima mazao ya chakula, mboga, matunda na viungo ili kutosheleza soko la ndani likiwemo la utalii sambamba na kuongeza pato la Taifa.

12. **Mheshimiwa Spika,** Uzalishaji wa viazi vitamu umeongezeka kutoka tani 46,586.61 kwa mwaka 2024 hadi kufikia tani 61,874.61 mwaka 2025. Aidha, kwa upande wa zao la muhogo, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 117,871.71 mwaka 2024 hadi tani 179,125.57 mwaka 2025. Vilevile, uzalishaji wa mboga na matunda umeongezeka kutoka tani 80,044.22 mwaka 2024 hadi kufikia tani 87,352.37 mwaka 2025 ikiwa ni tofauti ya tani 7,308.15. Hali hii imetokana na wananchi wengi kuhamasika na fursa za kilimo-biashara kwenye tasnia ya mazao ya matunda, mboga na viungo. Kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka umeongezeka kutoka tani 382,929.24 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 500,352.51 mwaka 2025 kwa tofauti ya tani 117,423.27. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa huduma za kilimo pamoja na muitikio mzuri wa wakulima katika kujifunza mbinu bora za uzalishaji.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa zao la biashara la karafuu, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 1,167.4 mwaka 2024 hadi kufikia tani 5,615.05 za mwaka 2025. Hali hii imetokana na kuufikia mwenendo wa msimu mkubwa wa uzalishaji pamoja na uwepo wa mvua za kutosha. Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha 'Mpango wa Kuendeleza Zao la Karafuu' pamoja na kuhamasisha wakulima wa zao hili kuongeza juhudi katika uzalishaji wenye tija kwa kuwapatia miche bora na elimu ya usimamizi wa zao la karafuu.

14. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mazao ya mifugo, takwimu zinaonesha ongezeko la uzalishaji wa maziwa kutoka lita 3,092,157 mwaka 2024 hadi lita 3,257,483 mwaka 2025. Aidha, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai 22,089,658 (Trei 736,321.9) mwaka 2024 hadi mayai 29,861,934 (Trei 995,397.8) mwaka 2025 **(Kiambatanisho Nam. 2A)**. Vilevile, takwimu za uchinjaji wa ng'ombe zinaonesha ongezeko kutoka ng'ombe 31,953 mwaka 2024 hadi ng'ombe 33,252 mwaka 2025. Pia, idadi ya mbuzi na kondoo waliochinjwa imeongezeka kutoka 12,084 mwaka 2024 hadi 16,867 mwaka 2025 **(Kiambatanisho Nam. 2B)**. Kadhalika, idadi ya kuku waliochinjwa imeongezeka na kufikia kuku 1,472,903 mwaka 2025 ikilinganishwa na kuku 1,085,856 mwaka 2024 **(Kiambatanisho Nam. 2C)**. Hata hivyo, uchinjaji wa wanyama wengine umeripotiwa kupungua wakiwemo bata kutoka 3,626 mwaka 2024 hadi bata 3,435 mwaka 2025, simbilisi na sungura 571 mwaka 2024 hadi 468 mwaka 2025 **(Kiambatanisho Nam. 2D)**.

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mazao ya misitu, takwimu zinaonesha kuwa matumizi ya kuni ndani ya Zanzibar yameongezeka kutoka mita za ujazo 18,764.50 mwaka 2024 hadi kufikia mita za ujazo 28,540.99 mwaka 2025. Aidha, matumizi ya mkaa nayo yameongezeka kutoka tani 1,665 mwaka 2024 hadi tani 2,411.10 mwaka 2025. Matumizi ya boriti (majengo) yamepungua kutoka mita za ujazo 2,254.53 mwaka 2024 hadi 1,691.27 mwaka 2025. Aidha, uzalishaji wa mapau ya kuezekea umeongezeka kutoka mita za ujazo 1,453.26 mwaka 2024 hadi kufikia mita za ujazo 2,843.09 mwaka 2025. Uzalishaji wa nguzo kubwa nao umeongezeka kutoka mita za ujazo 1,259 mwaka 2024 hadi kufikia mita za ujazo 2,256.31 mwaka 2025 **(Kiambatanisho Nam. 3)**.

## B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZOCHINI YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO.

16. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo imejiwekea vipaumbele vifuatavyo:

    a. Kuimarisha hifadhi na upatikanaji wa chakula nchini kunakozingatia uendelezaji wa mifumo ya chakula inayohimili mabadiliko ya tabianchi, kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji, usarifu na matumizi endelevu ya chakula;

    b. Kuendeleza miundombinu na uwezo wa tafiti za kilimo, maliasili na mifugo; ikijumuisha ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, na kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuimarisha maeneo ya karantini;

    c. Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu kwa manufaa ya jamii; ikiwemo uwekezaji katika miradi rafiki kwa mazingira yenye tija kwa umma;

d. Kuendeleza utoaji wa huduma za matrekta, zana za kilimo na pembejeo kwa wananchi; ikiwemo kushajiisha sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma hizo; na

e. Kuandaa na kusimamia mipango ya kisekta pamoja na kuimarisha mazingira mazuri ya watumishi.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA.

### Mapato yaliyokusanywa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

17. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ilikadiriwa kukusanya mapato ya **TZS bilioni 8.241** kupitia vyanzo vyake 11 viliopo Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya **TZS bilioni 6.272** zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 76 ya makadirio ya mwaka na ni asilimia 105 ya makadirio (**TZS bilioni 5.963**) ya Julai hadi Machi, 2026 **(Kiambatisho Nam. 4).**

### Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/27 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:

a. Kuzinduliwa kwa Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo Zanzibar (2025 – 2035) ambao utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka huu wa bajeti;

b. Kukamilisha Mfumo wa Kilimo App na kuanza usajili wa wakulima wa Zanzibar, lengo ni kurahisisha upatikanaji wa huduma za kilimo ikiwemo uratibu wa pembejeo;

c. Kukamilisha Mfumo wa Kusimamia Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini kwa sekta zote za kilimo. Wizara ipo katika hatua za kuufanyia majaribio kabla ya kuuzindua;

d. Kukamilisha ujenzi wa Maabara Mpya ya Utafiti wa Magonjwa ya Mifugo ambayo tayari imezinduliwa na imeanza kazi; na

e. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha masoko ya mazao ya nyuki katika eneo la Chamanangwe - Pemba.

19. **Mheshimiwa Spika;** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

a. Upungufu wa wataalamu kwa kada za kilimo, mifugo na maliasili kutokana na kushindwa kujaza mapengo ya wataalamu wanaostaafu au kuhamishiwa sekta nyengine;

b. Athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo uhaba wa mvua, matukio ya maradhi na wadudu waharibifu wa mazao, matukio ya moto wa msituni pamoja na upungufu wa malisho kwa mifugo;

c. Uvamizi mkubwa wa maeneo ya kilimo, mifugo na hifadhi za misitu unaopelekea uharibifu, upungufu wa eneo la misitu, vihatarishi kwa vyanzo vya maji na upungufu wa bioanuai muhimu;

d. Muamko mdogo kwa watumiaji wa pembejeo hatarishi kwa mazingira kunakopelekea athari hasi kwa mazingira, afya ya udongo na binaadamu; na

e. Matukio yaliyokithiri ya uharibifu na wizi wa mazao ya kilimo, maliasili na mifugo.

20. **Mheshimiwa Spika;** Katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

a. Kuwasilisha mapendekezo ya uajiri kwa kada tofauti Ofisi Kuu ya Utumishi Serikalini na vibali vya ajira tayari vimeanza kutolewa;

b. Wizara inatekeleza miradi yenye mnasaba na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo mradi wa uhimilivu wa mifumo ya chakula, mradi wa kuimarisha mifumo ya chakula kwa kuongeza tija, mradi wa kuendeleza mifumo ya chakula matumizi na urejeshaji wa ardhi, mradi wa mageuzi ya uzalishaji wa maziwa unaozingatia mabadiliko tabianchi pamoja na mradi wa ulinzi wa misitu ya mwambao kwa manufaa mchanganyiko;

c. Kuendeleza ushirikiano na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kufanya doria za pamoja katika maeneo ya kilimo, mifugo na misitu na kuimarisha vizuizi vya barabarani ili kudhibiti mwenendo wa wizi wa mazao ya kilimo na mifugo; na

d. Kuimarisha Divisheni ya Utibabu na Uhifadhi wa Mimea kwa ujenzi wa maabara mpya za udhibiti wa wadudu na magonjwa ya mimea pamoja na kuifanyia mapitio ‘Kanuni ya Uhifadhi wa Mimea na Usimamizi wa Viatilifu’ itakayozingatia utoaji wa taaluma kwa watumiaji wa viatilifu vya kilimo na mifugo.

## Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa Kipindi cha Julai 2025 – Machi 2026.

### Programu za Wizara

21. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilikusudia kutekeleza Programu Kuu nne (4) na Miradi 14 ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Programu Kuu nne (4) na Miradi 11 ya Maendeleo imetekelezwa. Programu zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:

    i. Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
    ii. Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;
    iii. Programu ya Maendeleo ya Mifugo; na
    iv. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

Aidha, Miradi 11 ya Maendeleo iliyotekelezwa ni:

i. Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji;
ii. Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula;
iii. Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa kukuza uchumi jumuishi (Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba);
iv. Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania – Kilimo P4R;
v. Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji;
vi. Mradi wa Kuimarisha usimamizi wa hifadhi ya akiba ya Ufufuma-Pongwe;
vii. Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC);
viii. Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na misitu;
ix. Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na kuhakikisha usalama wa Chakula (STREPHIT);
x. Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR; na
xi. Mradi wa Mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi.

22. **Mheshimiwa Spika,** Miradi mitatu (3) ya maendeleo, miwili (2) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (USAID) na mmoja (1) kutoka SMZ, imeshindwa kutekelezwa kutokana na kutokukamilika kwa taratibu za upatikanaji wa fedha.

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ilikusudia kutekeleza shabaha zifuatazo:

    a. Kuendelea Kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Wizara;

b. Kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, maliasili na mifugo ikiwemo ujenzi wa vituo viwili vya kutolea huduma kimoja Unguja na Kimoja Pemba;

c. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ikiwemo ndizi na mpunga, mboga na matunda, asali na uzalishaji wa mazao ya mifugo kwa kufanya tafiti, utaalamu na usambazaji teknologia kwa wakulima.

d. Kuendeleza utoaji wa huduma za ukulima na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na ushajiishaji wa sekta binafsi;

e. Kuimarisha upandaji wa miti kwa kuotesha miche 1,700,000 ya Misitu, Mikarafuu, Minazi, Matunda na Viungo na kutathmini hali ya uhuishaji wa miti iliyopandwa;

f. Kuimarisha usimamizi wa misitu pamoja na kuendeleza uwekezaji wa Miradi yenye tija katika hifadhi za misitu;

g. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya kazi; na

h. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi, ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za kisekta.

### Programu ya Maendeleo ya Kilimo

24. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu ndogo nne zifuatazo:

i. Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji;
ii. Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula;
iii. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar – ZALIRI; na
iv. Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

### *Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji*

25. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

a. Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde sita (6) ya Kibokwa, Kinyasini, Kilombero, Mlemele, Chaani na Cheju mabonde haya yote kwa sasa yanatumika;

b. Kukamilisha mafunzo 30 (16 kwa Kamati na 14 kwa Wakulima) ya uendeshaji wa mabonde yote ya Umwagiliaji, ambapo jumla ya wakulima 1,359 (662 wanawake na 697 wanaume) walinufaika; na

c. Kukamilisha mafunzo ya usimamizi na uongozi wa jumuiya, utunzaji wa kumbukumbu, ukarabati pamoja na taratibu za ukulima kwa vitendo (Shamba

darasa) kwa wakulima 590 (269 wanawake na 321 wanaume) waliowakilisha mabonde yote ya umwagiliaji. Aidha, mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa skimu kwa Mabibi na Mabwana shamba 26 (Wanawake 24 na Wanaume 2) yamefanyika.

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo hii iliomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 24.371** kati ya hizo **TZS bilioni 2.11** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 1.549** Mishahara na **TZS milioni 567** kwa matumizi mengineyo). Aidha, **TZS bilioni 22.056** kwa ajili ya Miradi kutoka washirika wa maendeleo na **TZS millioni 200.00** kutoka SMZ. Hadi kufikia Machi, 2026 Programu hii imepata **TZS bilioni 11.599**. Kati ya fedha hizo **TZS bilioni 1.017** kwa Mishahara, **TZS milioni 63.5** kwa matumizi mengineyo na **TZS bilioni 10.518** kwa kazi za maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

### *Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.*

27. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

a. Kukamilisha Tathmini ya Uzalishaji wa Zao la Mpunga kwa mwaka 2025 ambayo imeonyesha ongezeko kutoka tani 41,402 mwaka 2024 hadi tani 46,010 mwaka 2025;

b. Kuendeleza ukarabati wa Maghala 8 (5 Pemba na 3 Unguja) ya kuhifadhia chakula ambapo maghala 5 ya Pemba yamekamilika kwa wastani wa asilimia 85 na maghala 3 ya Unguja kwa wastani wa asilimia 15. Ukarabati kwa Maghala ya Unguja umeathiriwa na mabadiliko ya utoaji wa fedha za awali (advance payment) kwa wakandarasi;

c. Katika kudhibiti wadudu waharibifu kwenye mazao jumla ya wakulima wa mpunga 340 wa bonde la Cheju wamepatiwa huduma ya chambo chenye sumu ambapo kilo 2.5 ya sumu aina ya **Zinc phosphid** ilitumika na kiasi cha eka 2,751 za mpunga zimeweza kuokolewa kutokana na janga la panya;

d. Jumla ya miche 830,652 imezalishwa ikiwemo mikarafuu 336,703 (44,200 Unguja na 292,503 Pemba), minazi 16,200 (900 Unguja na 15,300 Pemba) pamoja na miche ya matunda 1,926,862 (Unguja 1,798,475 na 128,387 Pemba);

e. Kampeni za kudhibiti nzi waharibifu wa matunda zimefanyika ambapo jumla ya mitego 6,472 yenye kiwatilifu cha kunasia nzi wa matunda aina ya (ME) imepelekwa kwa wakulima mbalimbali; na

f. Jumla ya tani 205,900 za mazao zimekaguliwa kwa kuingizwa na kusafirishwa nje ya nchi. Kati ya hizo jumla ya tani 192,877 zimeingizwa ndani ya nchi na tani 13,023 zimesafirishwa kwenda nje ya nchi.

28. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo hii iliomba kuidhinishiwa jumla ya **TZS bilioni 29.908** kati ya hizo **TZS bilioni 5.152** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 4.401** kwa Mishahara na **TZS milioni 750.846** kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu iliombewa **TZS bilioni 24.756** kwa miradi ya maendeleo (**TZS billion 20.00** kutoka SMZ na **TZS bilioni 4.756** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2026 Programu hii imepata **TZS bilioni 17.234** (**TZS bilioni 8.533** ni Mishahara na **TZS bilioni 2.297** kwa matumizi mengineyo), na kwa fedha za Maendeleo zilizopatikana ni **TZS bilioni 6.404** (**TZS bilioni 1.756** kutoka SMZ na **TZS bilioni 4.648** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

### Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu

29. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu hii Ndogo kwa Mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya watalii 60,473 walitembelea misitu ya hifadhi wakiwemo (46,164 nje na 14, 309 ndani). Aidha, TZS 1,193,155,413 na Dola za Marekani 106,106, zilikusanywa ikiwa ada za viingilio;

b. Jumla ya miche 493,478 (269,243 Unguja na 224,235 Pemba) imeoteshwa kupitia vitalu 8 vilivyo chini ya Idara ya Misitu. Miongoni mwa miche hiyo ni ya misitu 411,522 na ya matunda na viungo 90,798. Aidha, miche 802,793 (637,173 misitu 165,620 ya Mikoko imeoteshwa katika vitalu Binafsi Unguja na Pemba. Miche hiyo inaendelea kupandwa katika kipindi hiki cha msimu wa mvua za masika;

c. Jumla ya hekta 40.31 zimepandwa miti hadi kufikia Machi 2026; Kati ya hizo, hekta 31.31 zimepandwa miti ya mikoko (9.81 Unguja na 21.5 Pemba). Aidha, hekta 9 zimepandwa miti ya misitu katika mashamba ya Serikali ya Chaani-Masingini, Dunga, Kibele na Maziwan'gombe;

d. Andiko la Mradi wa kupandisha hadhi msitu wa Mtambwe limekamilika na limewasilishwa kwa mfadhili na ameonesha nia ya kukubali kusaidia, utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha unaoanza Julai 2026;

e. Jumla ya Doria 390 (247 Unguja na 143 Pemba) zimefanyika katika maeneo ya rasimali za misitu ambapo matukio 134 (64 Unguja na 70 Pemba) yameripotiwa kuhusiana na uharibifu na ukataji wa misitu, usafirishaji wa mazao ya misitu bila ruhusa, uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa kilimo na ujenzi wa nyumba za makaazi, ukataji wa miti ndani ya hifadhi na matumizi mabaya ya misumeno ya moto; na

f. Uzalishaji wa asali unaendelea kushika kasi ambapo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya tani 19.26 (8.59 Unguja na 10.67 Pemba) zimezalishwa.

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2025/2026** Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu iliomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 7.460** kati ya hizo (**TZS bilioni 4.040** kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 2.606** Mishahara na **TZS bilioni 1.434** kwa matumizi mengineyo). Aidha, **TZS bilioni 3.420** kwa ajili ya Miradi ya maendeleo (**TZS bilioni 1.420** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **bilioni 2.000** kutoka SMZ ). Hadi kufikia Machi, 2026 Programu hii imepata **TZS bilioni 2.954** ambapo **TZS bilioni 1.834** kwa mishahara, **TZS milioni 613.826** kwa matumizi mengineyo na **TZS milion 505.932** za Miradi ya Maendeleo kutoka kwa washirika wa maendeleo.

### Programu ya Maendeleo ya Mifugo

31. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inatekelezwa kupitia Programu yake ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo.

### *Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo*

32. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu hii Ndogo kwa Mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya ng’ombe 2,047 (1,159 Unguja na 888 Pemba) wamepandishwa kwa njia ya sindano. Aidha, Jumla ya Mafunzo 10 yametolewa kwa wafugaji 307 wa ng’ombe, 190 wa kuku na 34 wa mbuzi. Vilevile, wafugaji 13,840 (7,044 Unguja na 6,830 Pemba) wametembelewa na kupewa ushauri wa kitaalamu;

b. Upandaji wa ekari nane na nusu (8.5) za malisho katika shamba la Kizimbani. Aidha, wafugaji 155 (103 Unguja na 52 Pemba) wamepatiwa mbegu za malisho kwa ajili ya mashamba yao. Vilevile, mashamba darasa 12 (7 Unguja na 4 Pemba) ya malisho yameanzishwa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba;

c. Katika jitihada za kudhibiti magonjwa ya wanyama, jumla ya kuku 206,553 (162,857 Unguja na 43,696 Pemba) wamechanjwa dhidi ya magonjwa ya kuku ikiwemo mahepe, gomboro na ndui; mbwa 6,271 (4,998 Unguja na 1,273 Pemba) dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na ng’ombe 431 (395 Unguja na 36 Pemba) dhidi ya ugonjwa wa mapele ya ngozi, ndigana kali, kimeta, chambavu na miguu na midomo; na

d. Sampuli 870 (719 Unguja na 151 Pemba) zilichunguzwa maradhi mbalimbali katika maabara ambapo sampuli 615 ziligundulikana na vimelea vya maradhi ya kuharisha damu na minyoo kwa kuku; ndigana kali, ugonjwa wa kiwele na minyoo kwa

ng'ombe; na minyoo na usugu wa vimelea vya maradhi dhidi ya madawa kwa mbuzi.

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo iliomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 11.463** kati ya hizo **TZS bilioni 3.713** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 3.016** Mishahara na **TZS milioni 697.067** kwa matumizi mengineyo). Aidha, **TZS bilioni 7.750** kwa ajili ya Miradi ya maendeleo (**TZS bilioni 5.250** kutoka washirika wa maendeleo na **TZS bilioni 2.500** kutoka SMZ). Hadi kufikia Machi, 2026 Programu Ndogo hii imepata **TZS bilioni 4.857**, ambapo **TZS bilioni 2.207** kwa mishahara na **TZS milioni 109.100** kwa matumizi mengineyo. Aidha kwa Miradi ya maendeleo programu hii imepata **TZS bilioni 2.541** (**TZS bilioni 1.726** kutoka SMZ na **TZS milioni 815.420** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

### Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo

34. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo;
ii. Mipango na Uratibu wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo; na
iii. Uratibu na Uendeshaji wa Ofisi Kuu Pemba.

#### *Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo*

35. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya TZS 108,698,567 zimetumika kuwapatia wafanyakazi 461 stahiki zao, ikiwemo ubani (67), likizo (247) na muda wa ziada (147);

b. Jumla ya wafanyakazi 153 wamepatiwa mafunzo (142 muda mrefu na 11 muda mfupi) katika fani mbalimbali; na

c. Wizara imewasilisha orodha ya maeneo sita (6) kwa ajili ya usajili na kuombewa hati za Umiliki wa Ardhi.

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji iliomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 2.909** kwa kazi za kawaida (**TZS bilioni 1.859** kwa Mishahara na **TZS bilioni 1.050** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2026 Programu Ndogo hii imepata **TZS bilioni 2.286** (**TZS bilioni 1.280** kwa mishahara na **TZS bilioni 1.006** kwa matumizi mengineyo).

### *Mipango na Uratibu wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo*

37. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo;

    a. Kuzinduwa Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (2025 -2035) ambao utekelezaji wake utaanza katika mwaka huu wa Bajeti;

    b. Kukamilisha Rasimu ya Sheria ya rasilimali za Mifugo ya mwaka 2026 ambayo imeshapitishwa na Baraza la Mapinduzi ikiendelea na taratibu nyengine za kisheria kabla ya kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi. Aidha, Waraka wa Mapitio ya Sera ya Kilimo ya mwaka 2026 umeshapitishwa na Kamati ya Makatibu Wakuu na sasa unapelekwa Baraza la Mapinduzi kwa Maamuzi; na

    c. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inaendelea na taratibu za utoaji wa matokeo ya Utafiti wa Kitaifa wa Sampuli za Kilimo ( National Agricultural Sample Survey).

38. **Mheshimiwa Spika** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii ndogo iliomba kuidhinishiwa **TZS milioni 739.426** kwa kazi za kawaida (**TZS milioni 384.426** Mishahara na **TZS milioni 355** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2026 Programu hii Ndogo imepata **TZS milioni 354.103** (**TZS milioni 297.603** kwa mishahara na **TZS milioni 56.500** kwa matumizi mengineyo).

### *Uratibu na Uendeshaji wa Ofisi Kuu Pemba*

39. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu hii Ndogo kwa mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

    a. Kuratibu vikao na ziara za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;

    b. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, vituoni na mashambani;

    c. Kuratibu ziara za wageni na viongozi pamoja na kuhudhuria katika vikao, sherehe na kumbukumbu za kitaifa; na

    d. Kutatua changamoto za wadau pamoja na kuimarisha mashirikiano na taasisi nyengine (za Serikali, Sekta binafsi, na Taasisi za Kijamii).

40. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii ndogo iliomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 4.601** kwa kazi za kawaida (**TZS bilioni 4.202** Mishahara na **TZS millioni 398.386** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2026 Programu hii Ndogo imepata **TZS bilioni 3.688** (**TZS bilioni 3.336** kwa mishahara na **TZS milioni 352.054** kwa matumizi mengineyo).

### Fedha Zilizopatikana kwa Kipindi cha Utekelezaji

41. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, iliomba kuidhinishiwa kutumia **TZS bilioni 92.728** kupitia Programu zake kuu nne, kati ya fedha hizo **TZS bilioni 23.27** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 18.018** kwa Mishahara na **TZS bilioni 5.252** kwa matumizi mengineyo). Aidha, **TZS bilioni 11.276** ikiwa ni Ruzuku (**TZS bilioni 8.531** kwa Mishahara na **TZS bilioni 2.745** kwa matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara iliombewa jumla ya **TZS bilioni 58.183** (**TZS bilioni 33.483** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **TZS bilioni 24.700** kutoka SMZ).

42. **Mheshimiwa Spika;** kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Wizara imepata **TZS bilioni 42.973** sawa na asilimia **46.34** ya fedha zilizoidhinishwa, kati ya hizo **TZS bilioni 16.361** zimetumika (**TZS bilioni 12.889** kwa mishahara na **TZS bilioni 3.471** kwa matumizi mengineyo). Aidha, ruzuku ya Serikali kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo, na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta ni **TZS bilioni 6.642** (TZS bilioni **5.616** kwa mishahara na **TZS bilioni 1.026** kwa matumizi mengineyo). Vilevile, kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Machi, 2026 Wizara imepata **TZS bilioni 23.682** (**TZS milioni 3.482** kutoka SMZ na **TZS bilioni 20.200** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) **(Kiambatanisho Nam. 5).**

### Utekelezaji wa Vipaumbele kwa Mujibu wa Mpango Mkakati wa Wizara na Taasisi

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ilisimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021 – 2026. Utekelezaji huo umesaidia kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ndogo za mazao, mifugo na maliasili.

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imetekeleza kwa majaribio Mpango wa Mageuzi wa Sekta ya Kilimo Zanzibar 2025 – 2035 kama ifuatayo;

    a. Utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula, Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania, Kuimarisha Mifumo ya Chakula

kwa Kuongeza Tija, pamoja na Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa Unaozingatia Mabadiliko Tabianchi;

b. Kuzinduliwa kwa Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo Zanzibar (2025 – 2035). Wizara kwa sasa inajipanga na utoaji wa uelewa na elimu juu ya Mpango huo ili kusaidia utekelezaji wake;

## D. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2025 - MACHI 2026.

45. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa faedha 2025/2026, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kupitia Taasisi zake mbili (2) imetekeleza majukumu yake yafuatayo;

### Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar – ZALIRI

46. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Taasisi hii kwa mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

a. Utafiti wa aina 4 za mbegu za mpunga zinazozaa mapema na kustahamili mabadiliko ya tabianchi umefanyika ambapo aina 2 za ZARIC 3 na ZARIC 5 zimeonesha mafanikio. Aidha, majaribio ya mbegu chotara ya WDR73 imeonyesha uwezo mkubwa wa kustahamili ukame;

b. Utafiti wa mbegu 10 za muhogo umefanyika ambapo aina 3 za KBH2016B/020 (uzalishaji Tani 51.73), ZNZ2018/011 (uzalishaji Tani 43.56), na KBH2016B/087 (uzalishaji tani 43.03) zimeonesha mafanikio;

c. Utafiti wa Arborvirus, wanaosababisha magonjwa yanayoambukizwa baina ya binaadamu na wanyama kwa kupitia mbu, unaendelea kwa kukusanya Sampuli; na

d. Ujenzi wa Maabara Mpya ya Utafiti wa Afya ya Wanyama umekamilika kwa asilimia 100.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo n Mifugo Zanzibar iliomba kuidhinishiwa ruzuku ya **TZS bilioni 8.354** kati ya hizo (**TZS bilioni 6.913** Mishahara na **TZS bilioni 1.440** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2026 Taasisi hii imepata **TZS bilioni 4.813** (**TZS bilioni 4.485** kwa Mishahara na **TZS milioni 327.304** kwa matumizi mengineyo).

### Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo

48. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Wakala kwa Mwaka 2025/2026 ni kama ifuatavyo:

    a. Jumla ya ekari 4,883 (Unguja 2,643.25 na Pemba 2,239.75) za mashamba ya wananchi zimelimwa. Aidha, huduma nyengine zilizotolewa ni kuvuna ekari 532.25, kupanda ekari 23.25 na kuchavanga ekari 510.75;

    b. Matengenezo kwa matrekta 43 (26 Unguja na 17 Pemba) yamefanyika na yanayoendelea na utowaji wa huduma shambani; na

    c. Mafunzo ya utowaji wa huduma za matrekta na zana za kilimo kwa Vijana 60 yamefanyika ili kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika utowaji wa huduma hizo.

49. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo iliomba kuidhinishiwa ruzuku ya **TZS bilioni 2.922** kati ya hizo (**TZS bilioni 1.617** ni Mishahara na **TZS milioni 1.305** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, Wakala imepatiwa **TZS bilioni 1.829** ambapo (**TZS bilioni 1.131** kwa ajili ya Mishahara na **TZS milioni 698.187** kwa matumizi mengineyo).

## E. MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### Mwelekeo wa Mapato

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imekadiriwa kukusanya mapato ya **TZS bilioni 12.131** kupitia vyanzo vyake tisa (9) vilivyopo Unguja na Pemba **(Kiambatanisho Nam. 6A).**

### Mwelekeo wa Matumizi 2026/2027

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, inaomba kuidhinishiwa kutumia **TZS bilioni 181.818** kupitia Programu zake kuu nne (4), kati ya fedha hizo **TZS bilioni 24.384** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 17.200** kwa Mishahara na **TZS bilioni 7.184** kwa matumizi mengineyo). Aidha, **TZS bilioni 12.428** ni Ruzuku (**TZS bilioni 8.341** kwa Mishahara na **TZS bilioni 4.087** kwa matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo (**Kiambatanisho Nam. 6B).**

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Wizara inaombewa jumla ya **TZS bilioni 145.006,** kati ya hizo **TZS bilioni 58.456** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**TZS bilioni 17.443** Msaada na **TZS bilioni 41.014** Mkopo) na **TZS bilioni 86.550** kutoka SMZ (**Kiambatanisho Nam. 6B).**

### Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Wizara ya Kilimo Uwagiliaji Maliasili na Mifugo itatekeleza Malengo yafuatayo:

a. Kuendelea Kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Wizara;

b. Kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, maliasili na mifugo ikiwemo ujenzi wa vituo viwili vya kutolea huduma kimoja Unguja na Kimoja Pemba;

c. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ikiwemo ndizi na mpunga, mboga na matunda, asali na uzalishaji wa mazao ya mifugo;

d. Kuendeleza utoaji wa huduma za ukulima na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na ushajiishaji wa sekta binafsi;

e. Kuimarisha usimamizi wa misitu pamoja na upandaji wa miti ya misitu, mikarafuu, minazi, matunda na viungo na kuendeleza uwekezaji wa miradi yenye tija katika hifadhi za misitu;

f. Kujenga miundombinu ya utafiti wa mifugo Chamanangwe, Pemba ikiwemo maabara ndogo ya utafiti wa afya ya wanyama, mabanda ya utafiti wa kuku na mbuzi;

g. Kuendelea na tafiti za kilimo, mifugo na maliasili kwa lengo la usambazaji wa teknologia kwa wakulima;

h. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya kazi; na

i. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi, ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za kisekta.

## Mwelekeo wa Programu za Wizara

54. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027, Wizara inatarajia kutekeleza Programu Kuu nne (4) na Miradi 10 ya Maendeleo. Programu hizo ni kama ifuatavyo:

i. Programu ya Utawala na Uratibu wa Wizara ya Kilimo;
ii. Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
iii. Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu; na
iv. Programu ya Maendeleo ya Mifugo.

Aidha, Miradi ya Maendeleo itakayotekelezwa ni kama ifuatayo:

i. Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji;
ii. Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania – Kilimo P4R;
iii. Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula;
iv. Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa kukuza uchumi jumuishi;
v. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu na Uwezo wa Utafiti wa Kilimo, Maliasili na Mifugo;
vi. Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR;
vii. Mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Mimea (Botanical garden) na mashamba ya Serikali;
viii. Mradi wa Ulinzi wa Misitu ya Mwambao wa Zanzibar kwa Manufaa Mchanganyiko;
ix. Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu; na
x. Mradi wa Mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi.

## Programu ya Utawala na Uratibu wa Wizara ya Kilimo

### *Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo*

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a. Kuendelea kutoa maslahi ya Wafanyakazi 1,238 Unguja na Pemba ikiwemo ubani 120, likizo 557 na muda wa ziada kazini 561;

b. Kuwajengea uwezo wa kitaluuma wafanyakazi 510 - kwa masomo ya muda mrefu wafanyakazi 10 na muda mfupi Wafanyakazi 500;

c. Kuwapatia mafunzo ya kujiandaa na kustafu Wafanyakazi 20;

d. Kuratibu na kusimamia vyanzo 10 vya mapato;

e. Kuratibu shughuli za ukaguzi wa hesabu za ndani za Wizara; na

f. Kusimamia na kudhibiti mali za Serikali kwa upimaji wa mashamba manne (4) Unguja na Pemba na kuyapatia hatimiliki.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji inaomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 6.526** kwa kazi za kawaida (**TZS bilioni 6.020** kwa Mishahara na **TZS milioni 506.000** kwa matumizi mengineyo).

### *Mipango na Uratibu wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo*

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi iliyopo chini ya Wizara;

b. Kuimarisha ukusanyaji wa Takwimu za kisekta;

c. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za ndani, Kikanda na Kimataifa; na

d. Kuratibu shughuli za Urajis wa wagunduzi wa mbegu mpya za kilimo.

58. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti inaomba kuidhinishiwa TZS milioni 605.390 kwa kazi za kawaida (**TZS milioni 344.000** kwa mishahara na **TZS milioni 261.390** kwa matumizi mengineyo).

### *Uratibu na Uendeshaji wa Ofisi Kuu – Pemba*

59. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Uendeshaji wa Ofisi Kuu Pemba, itatekeleza shabaha yake kuu ya Kuratibu na kusimamia kazi za kilimo, umwagiliaji, maliasili na mifugo.

60. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu ndogo ya Uratibu na Uendeshaji wa Ofisi Kuu Pemba inaomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 1.273** kwa matumizi mengineyo.

### Programu ya Maendeleo ya Kilimo

### *Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji*

61. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji itatekeleza shabaha zifuatazo:

a. Kufanya mapitio ya Mpango Mkuu wa Umwagiliajimaji 2002 (Irrigation Master Plan);

b. Kufanya ukarabati wa misingi ya umwagiliaji maji;

c. Kufanya ukarabati wa visima na pampu katika mabonde ya umwagiliaji maji; na

d. Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji kwa njia ya matone (drip irrigation).

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu ndogo hii inaombewa kuidhinishiwa **TZS bilioni 45.153** kati ya hizo **TZS bilioni 1.966** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 1.548** Mishahara na **TZS milioni 418.069** kwa matumizi mengineyo). Aidha, **TZS bilioni 43.187** kwa ajili ya Miradi kutoka washirika wa maendeleo.

***Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula***

63. **Mheshimiwa Spika,** Program Ndogo hii inahusisha pia Huduma za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo (ZALIRI) pamoja na huduma za Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027, Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula itatekeleza shabaha zake kwa makundi matatu kama ifuatavyo:

***Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.***

a. Kuweka na kusimamia akiba ya chakula katika maghala;

b. Kuzalisha miche 1,100,000 - 200,000 ya minazi, 500,000 ya mikarafu (200,000 Unguja na 300,000 Pemba) na 400,000 ya matunda (200,000 Unguja na 200,000 Pemba);

c. Kuimarisha utoaji wa elimu kwa wakulima;

d. Kufanya tathmini ya uzalishaji wa mpunga;

e. Kusimamia uzalishaji wa mbegu bora za nafaka; na

f. Kudhibiti miripuko ya wadudu na maradhi ya mimea.

***Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar (ZALIRI).***

a. Kuendelea na tafiti 19 za kilimo, mifugo na maliasili (9 za kilimo, 8 za mifugo na 2 za maliasili); na

b. Kuimarisha miundombinu ya utafiti wa mifugo Chamanangwe, Pemba ikiwemo maabara ndogo ya utafiti wa afya ya wanyama, mabanda ya utafiti wa wanyama.

***Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo***

a. Kuendeleza utoaji wa huduma za Matrekta na zana za Kilimo kwa wakulima, taasisi za Serikali, sekta binafsi pamoja na kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kazi, vipuri na vilainishi; na

b. Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika utoaji wa huduma za Matrekta na zana za kilimo.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula inaomba kuidhinishiwa jumla ya **TZS bilioni 102.579** kati ya hizo **TZS bilioni 19.447** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 12.469** kwa Mishahara na **TZS bilioni 6.978** kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu inaombewa **TZS bilioni 83.132** kwa miradi ya maendeleo (**TZS billion 78.500** kutoka SMZ na **TZS bilioni 4.632** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

### Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a. Kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje ya nchi wanaotembelea hifadhi kutoka 64,000 hadi kufikia 100,000 kwa kuimarisha vivutio na kuhamasisha miradi ya uwekezaji katika maeneo ya hifadhi za misitu kwa lengo la kuongeza mapato;

b. Kuanzisha taratibu za upandishaji hadhi Msitu wa Mtambwe Kaskazini na Kusini kutoka Hifadhi Jamii na kuwa Hifadhi ya Serikali itakayoshirikisha jamii katika usimamizi;

c. Kuotesha miche 1,000,000 (800,000 Misitu na 200,000 Matunda na Viungo) na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahudumu 65;

d. Kuhamasisha na kupanda miti hekta 130 (Hekta 100 misitu ya Serikali, na Hekta 30 maeneo ya Mikoko) pamoja na kufanya tathmini ya hali ya ukuaji;

e. Kuendeleza na kutoa elimu kwa jamii na kuimarisha ulinzi kwa kufanya doria 500 katika maeneo ya Misitu ya Hifadhi na Misitu ya Jamii Unguja na Pemba kwa lengo la kupunguza matukio ya uharibifu; na

f. Kuongeza uzalishaji wa asali na mazao mengine ya nyuki kutoka tani 19 kufikia tani 25 kwa kutoa elimu bora ya ufugaji, utunzaji wa kumbukumbu na kuhamasisha kwa ugawaji wa vifaa vya kufugia nyuki.

66. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu inaomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 11.946** kati ya hizo **TZS bilioni 3.559** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 2.408** Mishahara na **TZS bilioni 1.151** kwa matumizi mengineyo). Aidha, **TZS bilioni 8.387** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (**TZS bilioni 5.550** kutoka SMZ na **TZS bilioni 2.837** Washirika wa Maendeleo).

### Programu ya Maendeleo ya Mifugo

#### *Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo*

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu ndogo hii ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

    a. Kupandisha ng'ombe 2,500 (1,500 Unguja na 1,000 Pemba) kwa njia ya sindano;

    b. Kupanda eka 10 za malisho katika shamba la malisho Kizimbani kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mbegu za majani ya malisho ya mifugo na kuanzisha mashamba darasa ya malisho kwa kila Wilaya;

    c. Kutoa mafunzo 20 (12 Unguja na 8 Pemba) ya mbinu bora za ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kuku kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao;

    d. Kuwatembelea wafugaji 20,000 (Unguja 11,000 na Pemba 9,000) na kuwapa ushauri juu ya ufugaji bora wa kisasa wenye kuleta tija kwa wafugaji;

    e. Kuchanja kuku 250,000 (180,000 Unguja na 70,000 Pemba) dhidi ya ugonjwa wa mahepe, gumboro na ndui, mbwa 8,500 (Unguja 5,500 na Pemba 3,000) dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na ng'ombe 10,000 (6,000 Unguja na 4,000) dhidi ya magonjwa chambavu, kimeta, ugonjwa wa mapele ya ngozi na ugonjwa wa miguu na midomo; na

    f. Kuchunguza sampuli 1,500 (1,000 Unguja na 500 Pemba) za maradhi ya mifugo.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo inaomba kuidhinishiwa **TZS bilioni 13.736** kati ya hizo **TZS bilioni 3.436** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS bilioni 2.752** Mishahara na **TZS milioni 683.680** kwa matumizi mengineyo). Aidha, **TZS bilioni 10.300** kwa ajili ya Miradi ya maendeleo (**TZS bilioni 7.800** kutoka washirika wa maendeleo na **TZS bilioni 2.500** kutoka SMZ).

## F. MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

69. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo itatekeleza vipaumbele vyake kama vifuatavyo;

    a. Kuimarisha hifadhi na upatikanaji wa chakula nchini kwa kusimamia Ukarabati wa Maghala; Kuimarisha Mifumo ya Chakula kupitia huduma za kisasa na himilivu katika kilimo; kukuza uchumi jumuishi; na mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi;

b. Kuendeleza miundombinu na uwezo wa tafiti za kilimo, maliasili na mifugo; ikijumuisha ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuimarisha maeneo ya karantini; pamoja na Matumizi na Urejesheaji wa ardhi;

c. Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu kwa manufaa ya jamii; ikiwemo uwekezaji wenye tija kwa umma katika miradi rafiki kwa mazingira kama vile Bustani ya Mimea (Botanic Garden), mashamba ya Serikali pamoja na usimamizi wa Misitu ya Mwambao wa Zanzibar;

d. Kuendeleza utoaji wa huduma za matrekta, zana za kilimo na pembejeo kwa wananchi; ikiwemo kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma hizo; na

e. Kuandaa na kusimamia mipango ya kisekta pamoja na kuimarisha maslahi ya watendaji.

### Muhtasari wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

70. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS bilioni 12.131** kupitia vyanzo vyake Unguja na Pemba.

71. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, inaomba kuidhinishiwa kutumia **TZS bilioni 181.818,** kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo zikijumuisha ruzuku ya **TZS bilioni 12.428** kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo pamoja na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

72. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza miradi Kumi (10) kama inavyoonekana kwenye **Kiambatanisho Nam. 7A – 7J.** Utekelezaji wa Miradi hiyo unaombewa **TZS bilioni 145.006** (**TZS bilioni 86.550** kutoka SMZ na **TZS bilioni 58.456** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Aidha, Wizara itatelekeza Programu Kuu nne kama zinavyoonekana katika **Kiambatanisho Nam 8.**

### Shukurani

73. **Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huu, sasa natumia nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili na mifugo; zikiwemo Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; Ofisi ya Rais – Ikulu; Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za

Mitaa na Idara Maalum za SMZ; Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji; Wizara ya Kazi na Uwekezaji; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi; Wizara ya Afya; Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo; Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale; na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

74. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani za pekee ziende kwenye Wizara na Taasisi zinazoshabihiana na Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa upande wa Tanzania Bara. Wizara na Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

75. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuyashukuru Mashirika binafsi ya ndani na nje ya nchi yakiwemo BoT, PBZ, TADB, CRDB, NMB, ADB, ZSTC, TAHA, Plant Biodefenders, UWAMWIMA, COSTECH, Community Forest Pemba, Milele Zanzibar Foundation, ENABEL, Taasisi ya PPIZ, TARI, TALIRI, TPHPA, Kampuni ya Utengenezaji wa mbolea ya Minjingu na TPRI. Tunazishukuru pia nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia kuendeleza sekta hii, zikiwemo Japan, China, Korea ya Kusini, Norway, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya Kilimo. Benki ya Dunia, IFAD, OPEC, Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), WWF, WFP, GEF, UNDP, JICA, ILO, UNIDO, UNCDF, UN Women, KOICA, IITA, IRRI, WCS, PASS, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Root and Shoot, Heifer International, Exim Bank ya Korea, FLI ya Ujerumani na World Vegetable Centre**.**

76. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru viongozi wa Wizara hii ninayoiongoza wakiwemo; Naibu Waziri Mhe. Dkt. Salum Soud Hamed, Katibu Mkuu – Ndugu Saleh Mohamed Juma, Afisa Mdhamini - Mhandisi Idris Hassan Abdullah, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Wizara na Bodi ya Ushauri Jozani pamoja na watumishi wote kwa juhudi zao, ushirikiano na ushauri walionipatia, jambo ambalo limeniwezesha kusimama hapa leo hii kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mwaka huu.

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima, niiombe Kamati yako kumuombea dua aliyekua Naibu Katibu Mkuu Dkt. Mohamed Dhamir Kombo kutokana na mchango wake mkubwa uliotukuka kwa Sekta ya Kilimo Zanzibar. Mungu amlaze mahala pema peponi – Amin.

Pia, nawapongeza kwa dhati viongozi wa Jumuiya za Wakulima na Wafugaji, Wakulima, Wafugaji, Watunza mazingira na Wadau wote wa Sekta za Kilimo, Maliasili na Mifugo

kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao, mifugo na rasilimali za misitu kunakozingatia mazingira.

78. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Viongozi Wateule wote wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri, Masheha, Vikosi vya SMZ na SMT na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri wanayoendelea kuyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa Hotuba hii ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, kwa wakati.

79. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho Waheshimiwa Wajumbe **nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.**




**MHE. SULEIMAN MASOUD MAKAME,**
**WAZIRI,**
**WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO, ZANZIBAR**

## G. VIAMBATANISHO


### Kiambatanisho Nam. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2024 -2025, Zanzibar

| Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga 2024 - 2025 - Zanzibar | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ZAO | 2024 | | 2025 | |
| | Eneo lillilopndwa (ekari) | Uzalishaji (tani) | Eneo lillilopndwa (ekari) | Uzalishaji (tani) |
| Muhogo | 20,080.36 | 117,871.71 | 30,515.43 | 179,125.57 |
| Mpunga wa juu | 24,565.35 | 29,767.46 | 25,170.40 | 33,327.91 |
| Irrigation | 5,749.77 | 11,634.50 | 4,975.50 | 12,682.41 |
| Migomba | 7,303.29 | 62,808.29 | 8,628.48 | 74,204.93 |
| V/vikuu | 2,876.68 | 14,383.40 | 3,197.06 | 15,985.30 |
| Majimbi | 2,031.05 | 7,758.61 | 2,610.27 | 9,971.23 |
| Minanasi | 1,369.97 | 8,219.82 | 1,581.80 | 9,490.80 |
| J/kunde | 2,702.70 | 1,351.35 | 3,864.24 | 1,932.12 |
| Mipapai | 480.48 | 5,765.70 | 832.33 | 9,987.96 |
| V/Vidogo | 6,655.23 | 46,586.61 | 8,839.23 | 61,874.61 |
| Mtama | 860.17 | 326.86 | 840.55 | 319.41 |
| N/nyasa | 1,082.12 | 519.42 | 1,270.95 | 610.06 |
| Mahindi | 4,009.17 | 2,004.58 | 4,842.59 | 2,421.30 |
| Mbaazi | 847.93 | 2,738.81 | 1,028.75 | 3,322.86 |
| Uwele | 323.07 | 64.61 | 112.75 | 22.55 |
| Maboga | 954.48 | 4,524.24 | 1,489.71 | 7,061.23 |
| Chooko | 1,361.38 | 544.55 | 1,619.65 | 647.86 |
| Tungule | 4,335.11 | 13,005.33 | 3,978.67 | 11,936.01 |
| Nyanya | 1,828.41 | 3,364.27 | 2,044.38 | 3,761.66 |
| Bilinganyi | 2,847.08 | 6,263.58 | 3,367.11 | 7,407.64 |
| Bamia | 3,121.54 | 5,743.63 | 3,099.52 | 5,703.12 |
| Mchicha | 3,002.68 | 5,524.93 | 3,031.08 | 5,577.19 |
| Tango | 2,829.26 | 5,658.52 | 2,865.93 | 5,731.86 |
| Tikiti | 1,983.24 | 23,798.88 | 2,841.74 | 34,100.88 |
| Pilipili | 1,467.15 | 2,699.56 | 1,709.81 | 3,146.05 |
| **Jumla** | **104,667.66** | **382,929.24** | **124,357.93** | **500,352.51** |


**Kiambatanisho Nam. 2A: Uzalishaji wa Mayai na Maziwa, 2025.**




**Kiambatanisho Nam. 2B: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchinjwa, 2025**




**Kiambatanisho Nam. 2C: Idadi ya Kuku waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2025**



**Kiambatanisho Nam. 2D: Idadi ya Wanyama Wengine waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2025.**



**Kiambatanisho Nam. 3: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2025.**



### Kiambatanisho Nam. 4: Ukusanyaji wa Mapato, Julai 2025 - Machi 2026

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2025/2026 | MAKADIRIO (JULAI 2025 - MACHI 2026) | MAKUSANYO HALISI (JULAI-MACHI) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | | | | | |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 2,890,000 | 70,000 | 145,000 | 207 |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 26,010,200 | 13,310,000 | 19,259,008 | 145 |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 74,514,700 | 49,940,700 | 45,782,716 | 92 |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 46,240,300 | 29,380,000 | 31,233,109 | 106 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 144,500,700 | 135,000,700 | 5,000,000 | 4 |
| 1422066 | ADA YA UINGIAJI WA WAGENI | 21,675,200 | 16,525,000 | 12,434,500 | 75 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 2,890,000 | 1,875,000 | 1,926,000 | 103 |
| 1422068 | ADAYA MAZAO YA MIFUGO | 794,700 | 303,700 | - | - |
| 1422126 | ADA YA MAZAO YA KILIMO | 722,500 | 497,500 | - | - |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 50,575,200 | 40,300,000 | 244,277,500 | 606 |
| | **JUMLA PEMBA** | **370,813,500** | **287,202,600** | **360,057,833** | **125** |
| **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA** | | | | | |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 26,000,000 | 5,913,000 | 25,920,497 | 438 |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 463,973,000 | 364,306,640 | 495,869,328 | 136 |
| 1422066 | ADA YA UINGIAJI WA WAGENI | 2,033,010,000 | 1,567,376,561 | 1,260,483,989 | 80 |
| | **JUMLA** | **2,522,983,000** | **1,937,596,201** | **1,782,273,814** | **92** |
| **IDARA YA KILIMO** | | | | | |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 14,450,000 | 8,500,000 | 2,354,000 | 28 |
| 1422048 | ADA YA UKAGUZI WA MAZAO | 255,766,554 | 175,000,000 | 195,276,981 | 112 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 21,675,100 | 21,675,100 | - | - |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 101,150,500 | 61,150,500 | 594,812,500 | 973 |
| | **JUMLA** | **393,042,154** | **266,325,600** | **792,443,481** | **298** |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO KIZIMBANI** | | | | | |
| 1422066 | ADA YA UINGIAJI WAGENI | 86,700,500 | 60,700,500 | 21,917,022 | 36 |
| 1423002 | MAUZO YA MAZAO NA MICHE | 21,675,100 | 11,600,000 | 4,079,800 | 35 |
| | **JUMLA** | **108,375,600** | **72,300,500** | **25,996,822** | **36** |
| **IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO** | | | | | |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 4,034,535,800 | 2,773,145,836 | 2,883,494,754 | 104 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 15,025,300 | 10,016,868 | 3,555,000 | 35 |
| | **JUMLA** | **4,049,561,100** | **2,783,162,704** | **2,887,049,754** | **104** |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | | | | |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA | 796,824,801 | 616,200,000 | 424,485,000 | 69 |
| **JUMLA** | | **796,824,801** | **616,200,000** | **424,485,000** | **69** |
| | **JUMLA UNGUJA** | **7,870,786,655** | **5,675,585,005** | **5,912,248,871** | **104** |
| | **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | **8,241,600,155** | **5,962,787,605** | **6,272,306,704** | **105** |

## Kiambatanisho Nam. 5: Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2025 Hadi Machi, 2026.

| Program | Jumla | Mshahara | Matumizi Mengineyo | Ruzuku | | Maendeleo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | M/Mengineyo | Mshahara | SMZ | Muhisani |
| **PL0101: Maendeleo ya Kilimo** | **28,832,861,023** | **3,934,102,131** | **1,334,500,000** | **1,025,491,126** | **5,616,390,850** | **1,756,334,590** | **15,166,042,326** |
| SL010101: Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji *(00000P001: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji)* | 2,090,068,336 | 1,017,248,836 | 63,500,000 | | | | 1,009,319,500 |
| *00000P032: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula* | 8,383,611,675 | | | | | | 8,383,611,675 |
| *00000P034: Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji* | 1,125,000,000 | | | | | 0 | 1,125,000,000 |
| SL010102: Utafiti na Mafunzo ya Kilimo na Mifugo- ZALIRI | 4,812,542,575 | | | 327,304,200 | 4,485,238,375 | | |
| SL010103: Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula | 4,187,853,295 | 2,916,853,295 | 1,271,000,000 | | | | |
| *00000P028: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula* | 1,756,334,590 | | | | | 1,756,334,590 | |
| *00000P035: Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na kuhakikisha usalama wa Chakula (STREPHIT)* | 1,120,611,151 | | | | | | 1,120,611,151 |
| *00000P039: Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa kukuza uchumi jumuishi (FAO)* | 3,527,500,000 | | | | | | 3,527,500,000 |
| *00000P040: Mradi wa Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Huduma Endelevu za Ugani wa Kilimo* | 0 | | | | | | 0 |
| *00000P041: Mradi wa Ujasiriamali wa Vijana kwa Mustakbali wa Sekta ya Kilimo* | 0 | | | | | | 0 |
| SL010105: Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | 1,829,339,401 | | | 698,186,926 | 1,131,152,475 | | |
| **PL0102: Maendeleo ya Rasilimali za Misitu** | **2,954,182,782** | **1,834,425,163** | **613,825,988** | | | | **505,931,631** |
| SL010201: Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu | 2,448,251,151 | 1,834,425,163 | 613,825,988 | | | | |
| *00000P036: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)* | 95,000,000 | | | | | | 95,000,000 |
| *00000P037: Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR* | 320,843,231 | | | | | | 320,843,231 |
| *00000P038: Mradi wa Kuimarisha usimamizi wa hifadhi ya akiba ya Ufufuma-Pongwe* | 90,088,400 | | | | | | 90,088,400 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *00000L051: Mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Mimea (Botanical Garden) na mashamba ya Serikali* | 0 | | | | | - | |
| **PL0103: Maendeleo ya Mifugo** | **4,857,193,131** | **2,207,106,000** | **109,100,250** | | | **1,725,567,021** | **815,419,860** |
| SL010301: Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 2,316,206,250 | 2,207,106,000 | 109,100,250 | | | | |
| *00000P029: Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu* | 1,726,817,021 | | | | | 1,725,567,021 | 1,250,000 |
| *00000P033: Programu ya Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa wafugaji wadogo (C-SDTP)* | 814,169,860 | | | | | | 814,169,860 |
| **PL0105: Mipango na Usimamizi wa Kilimo Maliasili na Mifugo** | **6,328,277,341** | **4,913,740,771** | **1,414,536,570** | | | | |
| SL010501: Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 2,286,226,440 | 1,280,244,220 | 1,005,982,220 | | | | |
| SL010502: Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 354,102,900 | 297,602,900 | 56,500,000 | | | | |
| SL010503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo - Pemba | 3,687,948,001 | 3,335,893,651 | 352,054,350 | | | | |
| **JUMLA KUU** | **42,972,514,277** | **12,889,374,065** | **3,471,962,808** | **1,025,491,126** | **5,616,390,850** | **3,481,901,611** | **16,487,393,817** |

### Kiambatanisho Nam. 6A: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2026/2027 |
|---|---|---|
| **OFISI YA UNGUJA** | | |
| **03: IDARA YA KILIMO NA USALAMA WA CHAKULA** | | |
| 14210107 | MAUZO YA BIDHAA | 840,000,000 |
| 14220127 | ADA ZA UKAGUZI | 730,600,000 |
| 14230146 | UUZAJI WA MICHE | 150,600,000 |
| | **JUMLA** | **1,721,200,000** |
| **04: IDARA YA MAENDELEO YA MISITU** | | |
| 14220171 | ADA ZA KIINGILIO | 2,840,500,000 |
| 14220258 | ADA ZA VIBALI | 800,300,000 |
| 14230146 | UUZAJI WA MICHE | 60,901,000 |
| | **JUMLA** | **3,701,701,000** |
| **05: IDARA YA MIFUGO** | | |
| 14220174 | KIBALI CHA KUSAFIRISHIA MIFUGO | 21,400,000 |
| 14220327 | ADA UTOAJI HUDUMA | 4,539,000,000 |
| | **JUMLA** | **4,560,400,000** |
| **07: TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO NA MIFUGO ZANZIBAR** | | |
| 14220171 | ADA ZA KIINGILIO | 104,900,000 |
| 14230145 | UUZAJI WA MBEGU | 25,980,000 |
| | **JUMLA** | **130,880,000** |
| **08: WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | |
| 14210125 | MAPATO YA MAZAO YA KILIMO | 400,000,000 |
| | **JUMLA** | **400,000,000** |
| | **JUMLA UNGUJA** | **10,514,181,000** |
| **OFISI YA PEMBA** | | |
| **03: IDARA YA KILIMO NA USALAMA WA CHAKULA** | | |
| 14210107 | MAUZO YA BIDHAA | 560,000,000 |
| 14210125 | MAPATO YA MAZAO YA KILIMO | 19,697,000 |
| 14220127 | ADA ZA UKAGUZI | 239,085,000 |
| 14230146 | UUZAJI WA MICHE | 1,500,000 |
| | **JUMLA** | **820,282,000** |
| **04: IDARA YA MAENDELEO YA MISITU** | | |
| 14220171 | ADA ZA KIINGILIO | 60,143,000 |
| 14220258 | ADA ZA VIBALI | 270,485,000 |
| | **JUMLA** | **330,628,000** |
| **05: IDARA YA MIFUGO** | | |
| 14220174 | KIBALI CHA KUSAFIRISHIA MIFUGO | 10,759,000 |
| 14220327 | ADA UTOAJI HUDUMA | 200,650,000 |
| | **JUMLA** | **211,409,000** |
| **08: WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | |
| 14210125 | MAPATO YA MAZAO YA KILIMO | 254,000,000 |
| | **JUMLA** | **254,000,000** |
| | **JUMLA PEMBA** | **1,616,319,000** |
| | **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | **12,130,500,000** |

## Kiambatanisho Nam. 6B: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027.

| Program | Makadirio | Mshahara | Matumizi Mengineyo | Ruzuku | | Maendeleo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | M/Mengineyo | Mshahara | SMZ | Muhisani |
| **P01: Utawala na Uratibu wa Kilimo Maliasili na Mifugo** | **8,404,830,150** | **6,364,000,000** | **2,040,830,150** | | | | **0** |
| S0101: Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 6,526,000,000 | 6,020,000,000 | 506,000,000 | | | | |
| S0102: Mipango na Uratibu wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 605,390,000 | 344,000,000 | 261,390,000 | | | | |
| S0103: Uratibu na Uendeshaji wa Ofisi Kuu Pemba | 1,273,440,150 | | 1,273,440,150 | | | | |
| **P02: Maendeleo ya Kilimo** | **147,731,993,800** | **5,676,000,000** | **3,308,498,800** | **4,087,112,740** | **8,341,357,260** | **78,500,000,000** | **47,819,025,000** |
| S0201: Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji | 1,966,068,500 | 1,548,000,000 | 418,068,500 | | | | |
| *M0402: Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji* | 3,473,750,000 | | | | | | 3,473,750,000 |
| *M4250: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula* | 39,713,525,000 | | | | | | 39,713,525,000 |
| S0202: Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula | 7,018,430,300 | 4,128,000,000 | 2,890,430,300 | | | | |
| *M0457: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula* | 75,500,000,000 | | | | | 75,500,000,000 | |
| *M0429: Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa kukuza uchumi jumuishi (FAO)* | 4,631,750,000 | | | | | | 4,631,750,000 |
| H020204: Utafiti na Mafunzo ya Kilimo na Mifugo-ZALIRI | 9,752,870,000 | | | 2,881,080,000 | 6,871,790,000 | | |
| *M0551: Mradi wa Kuimarisha miundombinu na uwezo wa utafiti wa kilimo maliasili na mifugo* | 3,000,000,000 | | | | | 3,000,000,000 | |
| H20205: Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | 2,675,600,000 | | | 1,206,032,740 | 1,469,567,260 | | |
| **P03: Maendeleo ya Rasilimali za Misitu** | **11,945,796,064** | **2,408,000,000** | **1,150,840,800** | | | **5,550,000,000** | **2,836,955,264** |
| S0301: Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu | 3,558,840,800 | 2,408,000,000 | 1,150,840,800 | | | | |
| *M0401: Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR* | 841,730,264 | | | | | | 841,730,264 |
| *M0458: Mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Mimea (Botanic garden) na mashamba ya Serikali* | 5,550,000,000 | | | | | 5,550,000,000 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *M0550: Mradi wa Ulinzi wa Misitu ya Mwambao wa Zanzibar kwa Manufaa Mchanganyiko* | 1,995,225,000 | | | | | | 1,995,225,000 |
| **P04: Maendeleo ya Mifugo** | **13,735,680,250** | **2,752,000,000** | **683,680,250** | | | **2,500,000,000** | **7,800,000,000** |
| S0401: Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 3,435,680,250 | 2,752,000,000 | 683,680,250 | | | | |
| *M0026: Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu* | 2,500,000,000 | | | | | 2,500,000,000 | |
| *M0451: Programu ya Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa wafugaji wadogo (C-SDTP)* | 7,800,000,000 | | | | | | 7,800,000,000 |
| **JUMLA KUU** | **181,818,300,264** | **17,200,000,000** | **7,183,850,000** | **4,087,112,740** | **8,341,357,260** | **86,550,000,000** | **58,455,980,264** |

## Kiambatanisho Nam. 7A: Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 3.950 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo – Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia Mpango wa ROD/ODA, na TZS milioni 200 kutoka SMZ. Hadi kufikia Machi 2026 mradi umetumia TZS bilioni 3.528 kutoka kwa washirika wa maendeleo. |
| **Lengo Kuu la Mradi:** Kuchangia kuimarisha usalama wa chakula Zanzibar na kuongeza kipato cha wakulima wa mpunga kwa kuboresha uzalishaji. |
| **Malengo Mahsusi ya Mradi**<br>i. Kuboresha miundombinu ya kilimo (barabara, barabara za mashambani, sehemu za kuingilia matrekta, visima visima, uzio salama, ngome za ulinzi, sakafu ya kukaushia, vivuli vya trekta, hifadhi na vyoo) katika skimu sita (6) za umwagiliaji;<br>ii. Kutoa mashine za kilimo na vifaa vya usimamizi wa maji kwa Jumuiya za Wakulima na Wakala wa Serikali (GATFMS);<br>iii. Kuimarisha uwezo wa wakulima wa ndani, IFO, na maafisa ugani kupitia mafunzo ya shambani na programu za mwaliko nchini Korea;<br>iv. Kuanzisha na kuendesha Timu inayofanya kazi ya Usimamizi wa Mradi (PMT) kwa pamoja kati ya PMC na DOI kwa ajili ya uratibu na ufuatiliaji wa mradi; na<br>v. Kuhakikisha uendeshaji na usimamizi endelevu wa vifaa na vifaa vya mradi baada ya kukamilika kwa mradi. |
| **Malengo ya mwaka 2026/2027**<br>i. Kukamilisha kazi zilizobaki za ujenzi wa miundombinu ya kilimo katika skimu zote sita (6) za umwagiliaji;<br>ii. Kuhakikisha uendeshaji mzuri na matengenezo ya ghala iliyojengwa na vifaa vingine vya kusaidia;<br>iii. Kuendeleza programu za kuwajengea uwezo wakulima wa mpunga na maafisa ugani katika skimu zote;<br>iv. Kununua na kusambaza mitambo iliyobaki ya kilimo na vifaa vya usimamizi wa maji; na<br>v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya muda wa kati ya utendaji wa mradi. |
| **Kazi zilizotekelezwa mwaka 2025/2026**<br>i. Ununuzi na uwekaji wa vipengele vya miundombinu ya kilimo ikiwa ni pamoja na barabara za kuingilia, barabara za mashambani, sehemu za kuingilia matrekta, visima vya maji (Chaani), uzio wa usalama (Mlemele), na njia za ulinzi (Kinyasini, Chaani, Mlemele). ii. Ujenzi wa vifaa vya kuhifadhia (pamoja na vivuli vya trekta na vyoo) katika skimu sita (6) kote Unguja na Pemba;<br>ii. Utoaji na usambazaji wa mashine za kilimo (matrekta na zana) kwa GATFMS kwa wakulima ndani ya eneo la Mradi;<br>iii. Utekelezaji wa programu za mafunzo ya kuwajengea uwezo wakulima wa ndani, IFO, na maafisa ugani, ikijumuisha Programu ya Mafunzo ya Dakawa (kilimo cha mpunga, miundombinu ya umwagiliaji na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi); na<br>iv. Kuanzishwa na uendeshaji wa Timu ya Usimamizi wa Mradi (PMT) inayojumuisha wataalam wa PMC na maafisa wenzao wa DOI. |
| **Kwa mwaka 2026/2027:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 3.474 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo - Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia Mpango wa ROD(ODA). |

**Kazi zilizopangwa 2026/2027**

i. Kukamilisha kazi zilizobaki za ujenzi na ujenzi wa maghala na hifadhi katika skimu zote sita (6) za umwagiliaji;
ii. Kutekeleza awamu ya pili/tatu ya programu za kuwajengea uwezo wakulima, IFO, na maafisa ugani;
iii. Kufanya ziara za mafunzo na mafunzo ya makazi kwa wasimamizi wa maji katika chuo cha mafunzo maalumu Tanzania Bara - Imekamilika;
iv. Kununua na kupeleka vifaa vya ziada vya usimamizi wa maji (vifaa vya kupimia kiwango cha maji, vifaa vya kupimia pH) kwenye maeneo ya mradi;
v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya muhula wa kati (kukamilika kwa utafiti wa awali na ufuatiliaji wa kati); na
vi. Ili kuwezesha mpango wa mafunzo ya mwaliko nchini Korea kwa maafisa wa serikali na wahandisi waliohitimu (Ngazi ya Ufundi: watu 10).

## Kiambatanisho Nam. 7B: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania – Kilimo P4R

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha **2025/2026** mradi huu umetengewa jumla ya TZS bilioni 12.50 chini ya udhamini wa mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hadi kufikia **Machi 2026** mradi umetumia **TZS bilioni 8.384.** |
| **Malengo ya Mradi:**<br>i. Kusaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi; na<br>ii. Kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mifumo ya chakula. |
| **Maeneo Makuu ya Mradi:**<br>i. Kuongeza utoaji wa huduma za utafiti, mbegu na ugani<br>ii. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde manane (8); na<br>iii. Kufanya uratibu wa shughuli za Mradi. |
| **Shabaha kwa mwaka 2025/2026**<br>i. Kutafuta mjenzi na kuanza ukarabati wa majengo ya maabara;<br>ii. Kuendeleza tafiti za kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi;<br>iii. Kutafuta mjenzi na kuanza ukarabati wa vituo vya huduma kwa wakulima na miundombinu ya uzalishaji wa mbegu;<br>iv. Kufundisha maofisa ugani kuhusiana namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari;<br>v. Kutoa kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji, na teknolojia ya kilimo shadidi;<br>vi. Kukamilisha usarifu wa michoro kwa mabonde 16 ya umwagiliaji;<br>vii. kutafuta wajenzi na kuanza ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde 10 ya Bumbwisudi, Mtwango, Kianga, Kibokwa, Mwera, Makombeni, Tibirinzi, Weni, Saninga na Kinyakuzi; na<br>viii. Kuwafundishia vijana kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo. |
| **Kazi zilizotekelezwa 2025/2026**<br>i. Mjenzi kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya maabara za ZALIRI Kizimbani Unguja amepatika na ukarabati unategemewa kuanza karibuni;<br>ii. Mbegu bora mpunga ZARIC 3 na ZARIC 5 ambazo zinaweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi zimepatikana baada ya utafiti;<br>iii. Mjenzi kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya huduma kwa wakulima na miundombinu ya uzalishaji wa mbegu amepatika na ukarabati unategemewa kuanza karibuni;<br>iv. Jumla ya maofisa ugani 141 wamepatiwa mafunzo kuhusiana na namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya Habari;<br>v. Jumla ya wakulima 400 wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu bora za uzalishaji wa mpunga kwa kutumia teknolojia ya kilimo shadidi;<br>vi. Usarifu wa michoro kwa mabonde 16 umekamilika; na<br>vii. Jumla ya vijana 40 wamefundishwa namna ya kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo. |
| Kwa mwaka **2026/2027**: Mradi huu umepangiwa kiasi cha **TZS bilioni 39.714** Kutoka washirika wa maendeleo Benki ya Dunia. |

**Kazi zilizopangwa 2026/2027**

i. Kuanza ukarabati wa majengo ya maabara za ZALIRI Kizimbani Unguja;
ii. Kuendeleza tafiti za kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi;
iii. Kuanza ukarabati wa vituo vya huduma kwa wakulima na miundombinu ya uzalishaji wa mbegu;
iv. Kufundisha maofisa ugani kuhusiana namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari;
v. Kutoa kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji, na teknolojia ya kilimo shadidi;
vi. Kutafuta wajenzi na kuanza ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde 10 ya Bumbwisudi, Mtwango, Kianga, Kibokwa, Mwera, Makombeni, Tibirinzi, Weni, Saninga na Kinyakuzi; na
vii. Kuwafundishia vijana kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo.

## Kiambatanisho Nam. 7C: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu ulipangiwa kiasi cha TZS bilioni 20.0 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. Hadi kufikia Machi 2026 mradi umepata TZS bilioni 1.756 kutoka SMZ. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha kiwango bora cha akiba ya chakula kimkakati ili kuondoa uhaba wa chakula nchini na kukabiliana na mahitaji ya dharura ya chakula. |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:**<br>i. Ukarabati wa maghala chakavu 10;<br>ii. Ujenzi wa vihenge vyenye ujazo wa tani 80,000 Unguja na Pemba;<br>iii. Ununuaji wa mpunga kwa uhifadhi wa chakula cha akiba; na<br>iv. Ujenzi wa kituo cha uhifadhi wa chakula na Maabara kuu ya kilimo. |
| **Malengo ya mwaka 2026/2027**<br>i. Kukamilisha ukarabati wa maghala machakavu;<br>ii. Kujenga vehenge vyenye ujazo wa 50,000MT kwa Unguja na 30,000MT kwa Pemba; na<br>iii. Kujaza mpunga maghala yote yaliyokarabatiwa. |
| **Kazi zilizotekelezwa 2025/2026**<br>i. Ukarabati wa maghala 5 ya Pemba na 3 Unguja |
| **Kwa mwaka 2026/2027:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 75.500 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. |
| **Kazi zilizopangwa 2026/2027**<br>i. Kukamilisha ukarabati wa maghala matatu ya Unguja;<br>ii. Ujenzi wa vihenge Unguja na Pemba<br>iii. Ununuzi wa mpunga na kujaza maghala yaliyokwisha karabatiwa |

## Kiambatanisho Nam 7D: Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi (Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba)

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 1.442 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**FAO, ILO,UNCDF,UNIDO,UN Women)**. Hadi kufikia Machi 2026 mradi umetumia TZS bilioni 3.528 kutoka kwa washirika wa maendeleo. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kubadili mifumo ya chakula ili kuchochea Uchumi jumuishi, na kuongeza usalama wa chakula na lishe nchini |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:**<br>i. Kuimarisha minyororo ya thamani ya mazao ya chakula (migomba na mihogo) na mwani kwa kutumia mbinu jumuishi na zinazokabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; na<br>ii. Kuongeza ujuzi na uwezo wa vijana na wanawake katika kujiajili na kufikia fursa mbali kwenye sekta kilimo na miradi ya kijamii. |
| **Malengo ya mwaka 2026/2027**<br>i. Kusaidia wakulima upatikanaji wa mbinu mbali mbali zinazoendana na mabadiliko ya tabia nchi mfano miundombinu ya umwagiliaji na uzalishaji, vifaa vya uzalishaji mazao ya Bahari kwa kuchanganya na hasa mwenye maji ya kina kirefu na hii itapelekea upatikanaji wa aina tofauti za vyakula na kipato;<br>ii. Kuimarisha mbinu bora za uhifadhi wa mazao ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, kusaidia mbinu mbali mbali za usarifu wa mazao, kuongeza thamani, upatikanaji wa masoko na kuongeza uwezo wa ushindani kibiashara;<br>iii. Kusaidia mapitio ya sera na mikakati ili kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika mazao ya kipaombele;<br>iv. Kushajihisha teknolojia za kidijitali ili kusaidia uundaji na urasimishaji wa vikundi na vyama vya ushirika; na<br>v. kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo ya utoaji mikopo nafuu, pembejeo na teknolojia. |
| **Kazi zilizotekelezwa mwaka 2025/2026**<br>i. Kuwajengea uwezo wakulima 471 (wanawake katika kilimo bora cha migomba kupitia mbinu na technolojia zinazohimili mabadiliko ya tabia nchi;<br>ii. Kuanzisha mashamba 17 ya kibiashara ya migomba yenye ukubwa wa wastani wa ekari 1;<br>iii. Kujengea uwezo wakulima wa mwani 158 kutumia teknolojia jumuishi ya kilimo cha mwani pamoja na ufugaji wa majongoo bahari katika eneo moja;<br>iv. Kuboresha ujuzi wa Wakulima 52 pamoja na maafisa ugani 42 katika kutumia mbinu salama na jumuishi za usimamizi wa wadudu waharibifu (IPM) zinazozingatia usawa wa kijinsia;<br>v. Kuimarisha vyama 2 vya ushirika wa wakulima wa mwani (wanachama 57, kwa kupatiwa vifaa vya kuzuia upotevu wa mazao baada ya mavuno (uhifadhi, ukaushaji, na boti 2 za kuvunia);<br>vi. Kujengea uwezo vikundi vya wakulima 26 na vyama 4 vya ushirika vyenye zaidi ya wanachama 2,000 kuhusiana na upangaji wa biashara, usimamizi wa fedha, na uhusiano na masoko;<br>vii. Kujengea uwezo wanawake 212 katika maswala mbali mbali ikiwemo huduma za malezi ya watoto, nishati safi, na huduma za kidijitali ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi; na<br>viii. Kujengea uwezo wakulima 789 kuandaa mikakati inayoongeza ushiriki na ushawishi wa wanawake katika kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi na katika michakato ya utawala(governance) wa masuala ya tabianchi. |

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2026/2027:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 4.632 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |
| **Kazi zilizopangwa 2026/2027**<br>i. Kununua vifaa ya umwagiliaji kwa mashamba 30 yenye ukubwa wa wastani wa ekari 1;<br>ii. Kuanzisha mashamba 20 ya mfano ya kilimo mchanganyiko cha mwani pamoja na ufugaji wa majongoo bahari katika eneo moja;<br>iii. Kusaidia upatikanaji wa mbegu bora za mwani;<br>iv. Kuwajengea uwezo wakulima 300 katika kilimo bora cha mihogo;<br>v. Kuanzisha mashamba 20 ya mfano ya uzalishaji wa zao la mihogo;<br>vi. Kununua vifaa na kutoa huduma za kuanzisha biashara kwa wanawake na vijana 700 ili wajishughulishe na biashara za kilimo na uongezaji thamani katika minyororo ya thamani ya mwani, majongoo bahari (sea cucumber), muhogo na ndizi;<br>vii. Kuanzisha vituo viwili vya huduma za malezi Pamoja na utoaji wa vifaa vinavyopunguza mzigo wa malezi ili kuboresha upatikanaji wa huduma za malezi kwa wanawake na vijana;<br>viii. Kununua vifaa vya kidijitali (tablet 10 na desktop 10) Pamoja na kuanzisha klabu za kujifunza kwa njia ya kidijitali ili kuwezesha matumizi ya huduma za kifedha na zisizo za kifedha zilizopo zinazozingatia usawa wa kijinsia;<br>ix. Kujengea uwezo vikundi 6 vya mwani katika masuala ya usarifu, kufungasha na kuongeza thamani kwa kuboresha miundombinu na kuwapa vifaa ili kuongeza ushidani wa kibiashara; na<br>x. Kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa vijana 200 na kuunganisha na taasisi za kifedha ili kukuza mbinu za biashara endelevu. |

## Kiambatanisho Nam 7E: Mradi wa Kuimarisha Miundombinu na Uwezo wa Utafiti wa Kilimo Maliasili na Mifugo

| |
|---|
| Huu ni Mradi mpya ambao unatarajiwa kuanza utekelezaji mwaka huu wa fedha. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha uwezo wa kufanya utafiti wa kilimo, maliasili na mifugo Zanzibar kupitia uanzishaji na uimarishaji wa maabara za utafiti, vituo vya utafiti na majaribio ya Wanyama. |
| **Malengo makhsusi ya mradi**<br>i. Kuimarisha maabara za utafiti wa magonjwa ya wanyama Unguja na Pemba;<br>ii. Kuanzisha na kuimarisha miundombinu ya utafiti na mabanda ya utafiti kwa ajili ya utafiti wa mbuzi, kondoo, ng'ombe, kuku na wanyama wengine kwa Unguja na Pemba;<br>iii. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya utafiti kwa wanyama wa majaribio wakiwemo guinea pigs, panya wakubwa na panya wadogo na Wanyama wengine, na<br>iv. Kuanzisha ofisi za uwekaji kumbukumbu (documentation centres) na kuimarisha mazingira ya ofisi za kufanyia kazi za utafiti. |
| **Malengo ya mwaka 2026/2027**<br>i. Kuimarisha uwezo wa kitafiti wa kimaabara kwa magonjwa ya wanyama Chamanangwe, Pemba na kuweka mazingira mazuri ya ofisi za kufanyia kazi za utafiti kisiwani Pemba;<br>ii. Kuimarisha miundombinu ya utafiti wa mifugo kwa ikiwemo wa mabanda ya utafiti ya kuku na Sungura katika kituo cha utafiti wa mifugo Chamanangwe, Pemba, na<br>iii. Kuimarisha uwezo wa taasisi kufanya tafiti za mbuzi wa maziwa na nyama kwa kuwa na mabanda ya utafiti wa mbuzi katika kituo cha utafiti wa mifugo Chamanangwe, Pemba. |
| **Kwa mwaka 2026/2027:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni tatu (3) kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. |
| **Kazi Zilizopangwa kwa mwaka 2026/2027**<br>i. Ujenzi wa maabara ndogo ya utafiti wa magonjwa ya wanyama Chamanangwe, Pemba na kuweka mazingira mazuri ya ofisi za kufanyia kazi za utafiti kisiwani Pemba;<br>ii. Ujenzi wa mabanda ya utafiti ya kuku na Sungura katika kituo cha utafiti wa mifugo Chamanangwe, Pemba, na<br>iii. Ujenzi wa mabanda ya utafiti wa mbuzi katika kituo cha utafiti wa mifugo Chamanangwe, Pemba. |

## Kiambatanisho Nam. 7F: Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026:** Mradi huu ulipangiwa kutumia kiasi cha TZS bilioni 1.200 kutoka Wahisani wa Maendeleo – World Bank – GEF. Hadi kufikia Marchi 2026 Mradi huu Umeingiziwa TZS milioni 321. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Uendelezaji wa Mifumo ya chakula, Matumizi endelevu ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili katika maeneo yaliyoharibiwa |
| **Malengo ya mwaka 2026/2027**<br>i. Maendeleo ya usimamizi Jumuishi wa Mazingira kwa Kusimamia eneo lote la ardhi na rasilimali zake kwa namna ya kuunganisha maslahi ya watu na mazingira ili kuhakikisha rasilimali zinatumika kwa uendelevu na faida kwa kila mtu;<br>ii. Kukuza mbinu endelevu za uzalishaji wa chakula na minyororo ya thamani ya zao la mpunga yenye uwajibikaji; na<br>iii. Kufanya shughuli za Uhifadhi na Ukarabati wa Makazi ya Asili (Natural Habitats) kwa kulinda, kusimamia na kurejesha maeneo ya asili (misitu, ardhi oevu, mbuga na bahari) ili kuhakikisha viumbe hai(wanyama na mimea) wanaendelea kuishi, kuzaliana na kustawi. |
| **Kazi zilizotekelezwa 2025/2026**<br>i. Maendeleo ya usimamizi Jumuishi wa Mazingira kwa Kusimamia eneo lote la ardhi na rasilimali zake kwa namna ya kuunganisha maslahi ya watu na mazingira ili kuhakikisha rasilimali zinatumika kwa uendelevu na faida kwa kila mtu;<br>ii. Kukuza mbinu endelevu za uzalishaji wa chakula na minyororo ya thamani ya mpunga yenye uwajibikaji kwa kufanya mikakati mipana inayolenga kubadilisha namna mpunga unavolimwa, kusindika, na kuuzwa ili kulinda mazingira, kuongeza kipato cha wakulima, na kuhakikisha usalama wa chakula kwa sasa na vizazi vijavyo kwa kufanya yafuatayo:<br>o Kukuza mbinu Endelevu za uzalishaji kwa Kutunza Maji, Afya ya Udongo na mbolea, Udhibiti wa Wadudu na matumizi ya mbegu bora zinazostahamili magonjwa na mabadiliko ya tabianchi; na<br>o Minyoro ya thamani ya Mpunga yenye tija kwa kuanzia shambani(mbegu, mbolea) uzalishaji usindikaji (kukoboa) hadi kuuza. |
| **Kwa mwaka 2026/2027:** mradi umetengewa kiasi cha TZS milioni 841.730 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |
| **Kazi zilizopangwa 2026/2027**<br>i. Kukuza mbinu endelevu za uzalishaji wa chakula na minyororo ya thamani ya mpunga yenye uwajibikaji kwa kuwapatia maendeleo ya usimamizi Jumuishi wa Mazingira (Jukwaa Jumuishi) kwa Kusimamia eneo lote la ardhi la Kaskazini Unguja na rasilimali zake kwa namna ya kuunganisha maslahi ya watu na mazingira ili kuhakikisha rasilimali zinatumika kwa uendelevu na faida kwa kila mtu;<br>ii. Kufanya shughuli za Uhifadhi na Ukarabati wa Makazi ya Asili (Natural Habitats) kwa kulinda, kusimamia na kurejesha maeneo ya asili (misitu, ardhi oevu, mbuga na bahari) ili kuhakikisha viumbe hai (wanyama na mimea) wanaendelea kuishi, kuzaliana na kustawi; na<br>iii. Kuandaa Mipango ya Usimamizi na matumizi bora ya Ardhi na Maji kwa ngazi ya Shehia na Vijiji na kuwapatia mafunzo juu ya Mipango husika. |

### Kiambatanisho Nam 7G: Mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Mimea (Botanic garden) na mashamba ya Serikali

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 2.00 kutoka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2026, hakukuwa na fedha yoyote iliyopatikana kwa utekelezaji. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha utendaji na uzalishaji wa Shamba la Viungo la Kizimbani na kuanzisha bustani ya mimea (botanical garden) itakayosaidia utafiti wa kilimo, uhifadhi wa mimea, elimu kwa umma na utalii endelevu chini. |
| **Malengo makhsusi ya mradi**<br>i. Kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya viungo katika shamba kupitia matumizi ya mbinu bora za kilimo na teknolojia rafiki kwa mazingira;<br>ii. Kuanzisha na kuendeleza bustani ya mimea (botanical garden) kwa ajili ya uhifadhi wa aina tofauti za mimea ya asili na ile adimu;<br>iii. Kuimarisha miundombinu ya shamba na bustani ikiwemo vitalu, mifumo ya umwagiliaji, barabara za ndani na maeneo ya maonesho;<br>iv. Kukuza utalii wa kilimo (agro-tourism) kwa kuimarisha huduma za wageni na kuandaa vivutio vya kielimu na kitalii ndani ya shamba na bustani; na<br>v. Kuimarisha uhifadhi na usafi katika mashamba ya mikarafuu ya Wizara Unguja na Pemba. |
| **Kwa mwaka 2026/2027:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 5.550 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. |
| **Kazi Zilizopangwa kwa mwaka 2026/2027**<br>i. Ujenzi wa kituo cha taarifa na nyaraka kwa ajili ya spishi za mimea na elimu kwa wageni;<br>ii. Ukarabati wa ofisi za wafanyakazi na vyoo, pamoja na ujenzi wa vyoo vya ziada kwa wageni;<br>iii. Uchimbaji wa kisima kirefu (borehole) na uwekaji wa miundombinu ya kuhifadhi maji na umwagiliaji;<br>iv. Ujenzi wa jengo la mapokezi ya wageni na eneo la maegesho;<br>v. Ufungaji wa lango la kisasa la kuingilia;<br>vi. Ukarabati wa uzio wa waya (chain-link) ukikamilishwa na uzio wa miti hai yenye miiba (Caesalpinia);<br>vii. Uanzishaji wa sehemu ya chai na kahawa ya asili pamoja na eneo la mauzo ya bidhaa za viungo;<br>viii. Ziara za mafunzo katika bustani za mimea za Arusha na Nairobi kwa ajili ya kujifunza na kulinganisha (benchmarking);<br>ix. Upandaji wa miti ya kivuli na ujenzi wa vibanda vya kupumzikia;<br>x. Uanzishaji wa vivutio vya kiutalii kwa watalii wa ndani na nje;<br>xi. Ujenzi wa vituo vya kutolea huduma kwa watalii wa ndani na nje (migahawa, maduka ya fedha, bank, conference and recreation facilities na kadhalika) na<br>xii. Uanzishaji wa mashamba darasa (demonstration plots) kwa mazao ya viungo, mimea tiba na spishi adimu. |

### Kiambatanisho Nam 7H: Mradi wa Ulinzi wa Misitu ya Mwambao wa Zanzibar kwa Manufaa Mchanganyiko

| |
|---|
| Huu ni Mradi mpya ambao unatarajiwa kuanza utekelezaji mwaka huu wa fedha. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Ni kulinda makazi ya nchi kavu na ya pwani ya Zanzibar kwa manufaa mbalimbali kwa kutumia mbinu ya usimamizi wa kimandhari (landscape approach). |
| **Malengo makhsusi ya mradi**<br>i. Kusaidia Zanzibar kufuata mkondo wa maendeleo endelevu yenye uzalishaji mdogo wa hewa ukaa (carbon), kupitia utekelezaji bora wa mikakati na mipango ya kitaifa ya uhifadhi wa bayoanuwai na usimamizi wa matumizi ya ardhi;<br>ii. Kuboresha usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na misitu, ikiwemo kuimarisha uhusiano na maeneo yaliyo chini ya usimamizi wa misitu ya jamii (CFM), ili kulinda huduma muhimu za mifumo ya ikolojia pamoja na spishi za mimea na wanyama zenye umuhimu wa kimataifa, baadhi zikiwa ni za asili ya Zanzibar pekee;<br>iii. Kuchangia katika kudhibiti na kupunguza mwenendo wa uharibifu wa ardhi kwa kulinda makazi muhimu ya asili;<br>iv. Kupunguza uzalishaji wa gesi chafuzi (GHG) na kuongeza uwezo wa kuondoa hewa kutoka angani kupitia kupunguza ukataji wa misitu na kuhamasisha matumizi endelevu ya ardhi; na<br>v. Kukuza matumizi endelevu ya ardhi yakikamilishwa na hatua za ZASDP, zitakazochangia kupunguza umaskini, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza uwezo wa jamii za vijijini kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. |
| **Malengo ya mwaka 2026/2027**<br>i. Kuimarisha mfumo wa sera na taasisi wa Zanzibar kwa ajili ya usimamizi madhubuti wa bayoanuwai na mifumo ya ikolojia;<br>ii. Kuimarishwa kwa usimamizi wa mtandao wa maeneo yaliyohifadhiwa ya Zanzibar pamoja na maeneo yaliyo chini ya usimamizi wa misitu ya jamii; na<br>iii. Ujumuishaji wa masuala ya kijinsia na usimamizi wa maarifa.” |
| **Kwa mwaka 2026/2027:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 1.995 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |
| **Kazi Zilizopangwa kwa mwaka 2026/2027**<br>i. Kufanya mapitio ya kina ya sera na kanuni zilizopo (Misitu, Mazingira na Uchumi wa Buluu);<br>ii. Kufanya mashauriano na wadau katika Unguja na Pemba kuhusu mapungufu ya sera na changamoto za utekelezaji na usimamizi;<br>iii. Kufanya tathmini ya hali ya utekelezaji wa CoFMA 57 zilizopo;<br>iv. Kufanya mapitio na uidhinishaji wa miongozo ya CoFMA;<br>v. Uanzishaji wa CoFMA mpya; na<br>vi. Mafunzo na usaidizi wa kitaalamu katika uhifadhi. |

### Kiambatanisho Nam. 7I: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu ulipangiwa kiasi cha TZS Bilioni 2.500 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. Hadi kufika Machi 2026 mradi huu umeingiziwa TZS bilioni 1.727 kutoka SMZ na TZS milioni 1.250 kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Ujerumani – FLI. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha mazingira ya chinjio na karantini; kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen kwa ajili ya kuhifadhia mbegu za madume wa ng'ombe; na kudhibiti ndege waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo (kunguru); pamoja na kuimarisha maudhui ya Kilimo TV. |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:**<br>i. Kuimarisha miundombinu ya mifugo kwa kutoa huduma bora kwa jamii za wafugaji na wakulima;<br>ii. Kutoa elimu, teknolojia na mbinu bora za kilimo kwa wakulima kupitia maudhui ya TV; na<br>iii. Kutambua maeneo yenye makundi makubwa ya kunguru na kutekeleza shughuli za kuangamiza kunguru katika maeneo yaliyopewa kipaumbele. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2025/2026**<br>i. Kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen;<br>ii. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti Kizimbani – maabara, mabanda ya mbuzi na ofisi;<br>iii. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti wa mifugo Chamanangwe, Pemba ikiwemo maabara ndogo ya mifugo, mabanda ya utafiti ya kuku na mbuzi; na<br>iv. Kukarabati na kujenga miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba. |
| **Kazi zilizotekelezwa:**<br>i. Ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba unaendelea;<br>ii. Ujenzi wa maabara ya Utafiti wa Afya ya Wanyama kisiwani Unguja umekamilika; na<br>iii. Kazi ya ujenzi wa banda la utafiti wa mbuzi kisiwani Unguja umekamilika. |
| **Kwa mwaka 2026/2027** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS Bilioni **2.500** kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2026/2027**<br>i. Kukarabati na kujenga miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba;<br>ii. Kujenga uzio katika Karantini ya Donge Muwanda;<br>iii. Kujenga kliniki za mifugo mbili (2) (Maruhubi – Unguja na Wete – Pemba);<br>iv. Kukarabati Chinjio la Kisakasaka;<br>v. Kukarabati vituo (3) (Unguja 2 na Pemba 1) ya kutoa huduma za uzalishaji na utabibu wa mifugo (Animal Health and Production Center);<br>vi. Kudhibiti Wanyama waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo (kunguru);<br>vii. Kuzindua na kuimarisha maudhui ya Kilimo TV;<br>viii. Kufanya utambuzi wa kina kwa lengo la kubaini maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa kunguru, viota na mabadiliko ya tabia zao; na<br>ix. Kutengeneza na kuweka mitego kwa ajili ya kuwakamata kunguru katika maeneo yenye yaliopendekezwa. |

## Kiambatanisho Nam. 7J: Mradi wa Mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi

| |
|---|
| **Kwa mwaka wa fedha 2025/2026:** Mradi huu umetengewa jumla ya TZS **bilioni 5.250** Mkopo kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo IFAD na OPEC. Hadi kufikia Machi 2026 mradi umeshatumia TZS milioni 814.170 kwa utekelezai. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuchangia mabadiliko katika mnyororo wa thamani wa maziwa ili kuboresha maisha ya watu, kuongeza uhakika wa chakula, na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:.**<br>i. Kuimarishwa kwa uwezo na ustadi wa wakulima wadogo;<br>ii. Utoaji imara wa huduma muhimu za mifugo (afya ya wanyama, uzalishaji/uzazi, lishe, pembejeo) pamoja na ubunifu wa kiteknolojia;<br>iii. Kuimarishwa kwa uwezo wa vyama vya ushirika wa maziwa na wafugaji katika usimamizi wa biashara, pamoja na uelewa wa masuala ya kifedha;<br>iv. Mifumo ya ukusanyaji, uhifadhi, ujumuishaji na usafirishaji wa maziwa imeanzishwa na/au kuimarishwa, pamoja na matumizi ya maziwa na uelewa wa lishe yakihamasishwa;<br>v. Biashara ndogo na za kati za usarifu wa maziwa zinawezeshwa kwa huduma za maendeleo ya biashara na upatikanaji wa fedha; bidhaa na huduma za kifedha zilizobuniwa mahsusi, ikiwemo fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na bima, zinaandaliwa kwa wadau wa mnyororo wa thamani wa maziwa; na<br>vi. Mapitio na uboreshaji wa sera, mikakati na sheria za kitaifa unawezeshwa. |
| **Malengo ya mwaka 2026/2027**<br>i. Ununuzi wa vifaa vya uendeshaji (gari, mafuta, pikipiki, vifaa vya ofisini) na matengenezo yote zijumuishwe pamoja;<br>ii. Kuandaa wazalishaji katika ukusanyaji wa maziwa na kuwezesha ushirikiano wa uzalishaji;<br>iii. Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) pamoja na Usimamizi wa Maarifa (KM); na<br>iv. Usimamizi wa Mradi |
| **Kwa mwaka 2026/2027:** mradi umetengewa kiasi cha TZS **bilioni 7.800** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |
| **Kazi zilizopangwa 2026/2027**<br>i. Ujenzi wa rasilimali za uzalishaji kwa kaya zilizo katika mazingira magumu kupitia utoaji wa ng'ombe wa maziwa na msaada wa ujenzi wa mabanda ya ng'ombe;<br>ii. Kujenga uwezo wa wakulima wadogo kupitia Skuli za Wakulima wa Mifugo (FFS);<br>iii. Kutoa msaada wa huduma za ugani na huduma za afya ya mifugo;<br>iv. Kutoa msaada wa uzalishaji wa mbegu za malisho;<br>v. Kuongeza upatikanaji wa maji kwa mifugo;<br>vi. Kuongeza matumizi ya kidijitali ili kuboresha uzalishaji;<br>vii. Ufuatiliaji wa magonjwa, kampeni za chanjo na mfuko wa dharura;<br>viii. Uundaji na uimarishaji wa vikundi vya wazalishaji wa maziwa na vyama vya ushirika;<br>ix. Uanzishaji na ukarabati wa Vituo vya Kukusanyia Maziwa (MCCs); na<br>x. Uhamasishaji wa matumizi ya nishati bora na nishati jadidifu kwa ajili ya kupoza maziwa na usindikaji mdogo wa maziwa. |

**Kiambatanisho Nam. 8: Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Programu kwa Mwaka 2026/2027**

